القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

37. Ili Mwenyezi Mungu apate kuwapambanua walio wabaya na walio wazuri na kuwaweka wabaya juu ya wabaya wengine na kuwarundika wote pamoja na kuwatupa katika Jahanamu. Hao ndio waliokhasirika.

لِيَمِيزَ اللّٰهُ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ وَيَجْعَلَ الْخَبِيثَ
بَعْضَهُ عَلٰى بَعْضٍ فَيَرْكُمَهُ جَمِيعًا فَيَجْعَلَهُ
فِي جَهَنَّمَ ۚ أُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٣٧﴾

38. Waambie wale waliokufuru: "Kama wataacha (yale mabaya waliyokuwa nayo) watasamehewa yaliyopita, na wakiyarudia (tutawatesa kama tulivyowatesa wao mara zilizopita na kama tulivyoitesa hiyo mijikafiri mikubwa ya zamani); imekwisha kuwapitia mifano ya (mambo yaliyowapata) watu wa zamani."

قُلْ لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓا إِنْ يَّنْتَهُوا يُغْفَرْ لَهُمْ مَّا قَدْ
سَلَفَ ۚ وَإِنْ يَّعُودُوا فَقَدْ مَضَتْ
سُنَّتُ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٨﴾

39. Na piganeni nao (makafiri) mpaka yasiweko mateso (nyinyi kuteswa na wao kwa ajili ya dini kama wanavyokuteseni sasa); na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (asitaaradhiwe mtu kuabudu dini anayoitaka). Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

وَقٰتِلُوهُمْ حَتّٰى لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَّيَكُونَ الدِّينُ
كُلُّهُ لِلّٰهِ ۚ فَإِنِ انْتَهَوْا فَإِنَّ اللّٰهَ بِمَا يَعْمَلُونَ
بَصِيرٌ ﴿٣٩﴾

40. Na kama wakigeuka basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mola wenu, ni Mola Mwema na msaidizi Mwema (atakuhifadhini nao).

وَإِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمُوٓا أَنَّ اللّٰهَ مَوْلٰىكُمْ ۚ
نِعْمَ الْمَوْلٰى وَنِعْمَ النَّصِيرُ ﴿٤٠﴾

41. Na jueni ya kwamba chochote mnachokiteka (mnachokipata ngawira), basi sehemu yake ya tano ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume na jamaa (zake Mtume) na mayatima na masikini na wasafiri (walioharibikiwa); ikiwa nyinyi mumemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyoyateremsha kwa mja wetu siku ya kipambanuzi, siku (inayowafikiana na siku) yalipokutana majeshi mawili (siku ya vita vya Badri—jeshi la Waislamu na jeshi la makafiri). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye uweza juu ya kila kitu.

وَاعْلَمُوٓا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَأَنَّ لِلّٰهِ خُمُسَهُ
وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِينِ وَ
ابْنِ السَّبِيلِ إِنْ كُنْتُمْ اٰمَنْتُمْ بِاللّٰهِ وَمَآ أَنْزَلْنَا
عَلٰى عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعٰنِ ۗ
وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤١﴾

---

Wanayakataa katakata; hawayataki tu.

34. Katika mwaka wa 6 wa Al Hijra alitoka Mtume na baadhi ya Masahaba zake kuhiji; Maqureshi wakawazuilia. Wanajiona wao kuwa ndio wenyewe wenye amri ya Makka na hiyo Al Kaaba; kwa kuwa zimo katika mikono yao.

35. Maqureshi na makafiri wenziwao wakifanya ibada zao hapo katika Al Kaaba na kwengineko walikuwa wakipiga kofi kwa mikono yao na kuliza vikorombwe kwa mikono yao na ndimi zao. Basi huku kupiga kofi wakati wa ibada na kutoa sauti za mfano wa vikorombwe si jambo zuri hata kidogo.

36. Hao matajiri wa kikafiri, khasa Maqureshi, walitumia pesa nyingi kufanyia mambo na propaganda za kuuzuilia Uislamu usende mbele. Ikawa kazi yao bure—Uislamu umetawanyika ulimwengu mzima.

Na sasa pia hiyo mibwana mikubwa na midola mikubwa isiyokuwa ya Kiislamu inatumia chungu ya pesa na chungu ya propaganda ili kuuzuilia Uislamu usitapakae. Kumbe huo unatanda tu kidogo kidogo ulimwengu mzima kama alivyokariri kusema Mwenyezi Mungu katika Qurani kuwa Uislamu utatangaa tu hata wakichukia vipi makafiri.

42. (Kumbukeni) mlipokuwa kando ya bonde lililo karibu (na Madina), nao (wenye jeshi la makafiri) walikuwa kando yabonde lililo mbali, na ule msafara (wa Maqureshi uliokuwa una mali yao) ulipokuwa chini yenu (upande mwengine kabisa); na kama mngalipeana miadi mngalihitalifiana. Lakini (mumekutana vivi hivi na jeshi lao la vita) ili Mwenyezi Mungu alipitishe jambo lililokuwa lazima litendeke; kusudi yule aangamiaye (akakhitari ukafiri) aangamie kwa dalili zilizo dhahiri (alizokataa kuzifuata), na anayehuika (yaani anayefuata Uislamu) ahuike kwa dalili dhahiri. Na hakika Mwenyezi Mungu Mwenye kusikia Mwenye kujua

إِذْ أَنْتُمْ بِالْعُدْوَةِ الدُّنْيَا وَهُمْ بِالْعُدْوَةِ
الْقُصْوٰى وَالرَّكْبُ أَسْفَلَ مِنْكُمْ ۚ وَلَوْ تَوَاعَدْتُّمْ
لَاخْتَلَفْتُمْ فِي الْمِيعٰدِ ۙ وَلٰكِنْ لِّيَقْضِيَ اللّٰهُ أَمْرًا
كَانَ مَفْعُولًا ۙ لِّيَهْلِكَ مَنْ هَلَكَ عَنْ بَيِّنَةٍ
وَّيَحْيٰى مَنْ حَيَّ عَنْ بَيِّنَةٍ ۗ وَإِنَّ اللّٰهَ لَسَمِيعٌ
عَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

---

Bali na wale Waislamu wanaopenda mambo ya Bidaa, yasiwafurahishe mambo ya Suna ya Mtume; namna hao nao; wanatumia pesa zao nyingi na propaganda zao kubwa kutilia nguvu hizo bidaa na kupinga Suna; lakini ya Suna hayo kidogo kidogo yanatatua miguu kwenda.

38. Tumetaja mara nyingi rehema ya Mwenyezi Mungu juu ya viumbe vyake na namna anavyowapokea wanaporejea.

39. Tumebainisha mara nyingi kuwa upeo wa kukubalisha Uislamu kupigana ni huu: kusiwe watu kupingwa na kupigwa na kuuawa kwa ajili ya dini. Awe mtu huru kufuata dini atakayo. Na Wazungu ndio kwanza kuyajua haya kiasi cha miaka elfu mbili kupita baada ya kubainisha haya Uislamu.

41. Siku ya awali waliyokabiliana Waislamu na makafiri wakapigana—jeshi hili na jeshi hilo—ni siku ya Vita vya Badri. Vita vilipiganwa hapo Badri, mahala ambapo pako katikati baina ya Makka na Madina. Wakashindwa makafiri vibaya vibaya, na wakashinda Waislamu vizuri kabisa hata ikawa mpaka leo wanakumbukwa Islamu hao waliopigana vita hivyo. Wanajulikana kwa jina la Ahl Badr (Halalbadiri). Na watu wenyewe hao walikuwa kiasi cha watu mia tatu tu basi hivi. Lakini mara nyingi wachache wanaokuwa katika haki huwashinda wengi walio katika batili.

Na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa majina ya 'Ahl Badr' siyo njia iliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu. Alivyoamrisha Mwenyezi Mungu ni kumuomba kwa Majina Yake Matukufu kama vile 'Tayibal Asmai' na mfano wake. Ama ile inayoitwa 'wasila ambayo mwanzo wake ni 'Saaltuka ya Mawlaya' haifai kabisa kama tulivyobanisha katika Aya ya 180 ya *Suratul Aaraf.*

Vita hivi vilipiganwa mchana wa mwezi 17 Ramadhani mwaka wa 2 wa Al Hijra (mwaka wa pili wa kuhamia Mtume Madina).

Na kwa bahati hii siku ya mwezi 17 Ramadhani—kwa kiasi chamiaka 15 nyuma—ilikuwa ndiyo siku uliyomteremkia Mtume utume siku ya KIPAMBANUZI (kupambanua baina ya haki na batili.)

Basi wanakumbushwa Islamu, hapa zote neema mbili—neema ya kuletewa Mtume na neema ya kuwashinda maadui wa Mtume.

Kisha wanapewa habari ya kugawa ngawira waliyoipata—na watakazozipata. Inaambiwa ngawira sehemu TANO. Sehemu nne za 4/5 wagaiwe wale waliopigana. Na sehemu ile ya 5 wagaiwe wahitaji wa uma kama (a) Vijana wasiokuwa na wazee (mayatima), (b) Watu wazima wasiokuwa na kitu na hawajiwezi masikini, (c) Wenye kuharibikiwa katika nchi za ugeni, wanasaidiwa ili warejeshwe kwao.

Na ilivyokuwa mtu hapendi kutangaziwa ufakiri—na hapa wametangaziwa ufakiri wao—Mwenyezi Mungu ameona amtie na (a) Mtume na jamaa zake wanaomsaidia kutangaza dini katika kikundi hiki kilichoambiwa kipewe ile sehemu ya tano 1/5; ili ashirikiane nao, wasije wakavunjika moyo. Basi Mtume alikuwa anagawiana nao katika sehemu hii; akiwagaia humo hao jamaa zake waliokuwa wakiupigania Uislamu kwa jitihada zao.

Na Mwenyezi Mungu akajitia Mwenyewe katika hao ili kuzidi kuwaondoshea majonzi na kuwapa hishima mbele za watu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe yumo katika fungu lao hilo. Akasema:– Sehemu yake ya tano ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume na Jamaa na Mayatima na Masikini na Wasafari.

Basi hiyo sehemu iliyoambiwa ni ya Mwenyezi Mungu hutumiwa kwa mambo ya maslaha ya Uma.

42. Sehemu 3 hapa zimetajwa. Jeshi la waislamu. Jeshi la vita la makafiri Maqureshi na Msafara wa Maqureshi wa biashara.

43. (Kumbuka) Mwenyezi Mungu alipokuonyesha katika usingizi wako (kwamba wao makafiri) ni wachache; (mkapata nyoyo za kukabiliana nao). Na kama angalikuonyesha kwamba wao ni wengi mngalivunjika nyoyo na mngalizozana katika jambo hilo (kuwa tupigane nao au tusipigane nao). Lakini Mwenyezi Mungu akakulindeni (na hayo). Bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani (seuze yaliyo dhahiri).

إِذْ يُرِيكَهُمُ اللَّهُ فِي مَنَامِكَ قَلِيلًا ۖ وَلَوْ أَرَاكَهُمْ
كَثِيرًا لَّفَشِلْتُمْ وَلَتَنَازَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَلَٰكِنَّ
اللَّهَ سَلَّمَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٤٣﴾

44. Na (kumbukeni) alipokuonyesheni machoni mwenu mlipokutana kwamba wao ni wachache (ili mjasirishe kupigana nao); na akakufanyeni nyinyi kuwa wachache (mno kabisa) machoni mwao (waone upuzi kupigana kwa hima na watu wachache kama nyinyi. Mungu amefanya hayo) ili alitimize jambo aliloamrisha litendeke. Na mambo yote hurejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.

وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ إِذِ الْتَقَيْتُمْ فِي أَعْيُنِكُمْ قَلِيلًا
وَيُقَلِّلُكُمْ فِي أَعْيُنِهِمْ لِيَقْضِيَ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ
مَفْعُولًا ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٤٤﴾ ع

45. Enyi mlioamini! Mkutanapo na jeshi (la makafiri) kazaneni barabara (wala msikimbie) na mumkumbuke Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mpate kufaulu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ فِئَةً فَاثْبُتُوا
وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٤٥﴾

46. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala msizozane (msigombane), msije mkaharibikiwa na kupotea nguvu zenu, na vumilieni (msitahamiliane). Bila shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaovumilia.

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَنَازَعُوا فَتَفْشَلُوا وَ
تَذْهَبَ رِيحُكُمْ ۖ وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٤٦﴾

47. Wala msiwe kama wale waliotoka katika majumba yao (miji yao) kwa fakhari na kujionyesha kwa watu na kuzuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu. (Nao ni hao Maqureshi waliotoka Makka kuja Madina kumpiga Mtume). Na Mwenyezi Mungu ameyazunguka (kuyajua yote) wanayoyafanya.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ خَرَجُوا مِن دِيَارِهِم
بَطَرًا وَرِئَاءَ النَّاسِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ
اللَّهِ ۚ وَاللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿٤٧﴾

---

Maqureshi waliwataabisha Waislamu Makka muda wa miaka kumi na mitatu kwa kuwanyang'anya chao na kuwapiga na kuwaua pia. Mwisho wakakimbia Waislamu, wakenda Madina, wakaacha kila mali yao Makka; yakachukuliwa na hao makafiri. Na juu ya hivyo wakawa makafiri wanakuja Madina usiku, wakipitisha khasara kubwa kubwa; kisha wanakimbia. Kama khasara za kutia moto mitaa na wanyama; bali khasara za kukamata mateka na kuua pia.

Basi baada ya miaka kumi na mitano ya kutaabishwa hivi sasa Waislamu walipewea ruhusa na Mwenyezi Mungu wapigane nao makafiri kama wanavyowapiga, na wawanyang'anye ili warejeze baadhi ya khasara zao.

Basi akasikia Mtume kuwa kuna msafara wa mali nyingi wa Maqureshi utapita karibu na hapo Madina. Akawatia shauku Masahaba watoke pamoja naye wakaushambulie waunyang'anye mali yake. Wakamfuata watu kiasi cha mia tatu bila ya kuwa na zana za vita, kwani walikuwa hawajaazimia vita; wameazimia kuwanyang'anya mali yao tu hao watu wachache waliokuwa na msafara huo—hawakuwa na nia ya kuwaua.

Lakini mkubwa wa msafara huo kwa bahati alipata habari kuwa anafuatwa na Mtume na Masahaba zake ili wanyang'anywe mali hayo. Basi pale pale akageuza njia nyingine ambayo siyo inayopitwa kwa dasturi ili Mtume asikutane nao. Na akapeleka mjumbe Makka akawaambia watu wa Makka kuwa msafara utashambuliwa, basi nawaje upesi wauhami.

48. Na (kumbukeni) Shetani alipowapambia vitendo vyao (wale makafiri) na kusema: "Leo hakuna watu wa kukushindeni, na mimi ni mlinzi wenu," Lakini yalipoonana (yalipokutana) majeshi mawili, (Shetani) alirudi nyuma na kusema: "Mimi si pamoja nanyi, mimi naona msiyoyaona, mimi ninamuogopa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu."

وَإِذْ زَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَٰنُ أَعْمَٰلَهُمْ وَقَالَ لَا
غَالِبَ لَكُمُ الْيَوْمَ مِنَ النَّاسِ وَإِنِّي جَارٌ لَّكُمْ ۚ
فَلَمَّا تَرَآءَتِ الْفِئَتَانِ نَكَصَ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ وَقَالَ
إِنِّي بَرِيٓءٌ مِّنكُمْ إِنِّيٓ أَرَىٰ مَا لَا تَرَوْنَ إِنِّيٓ
أَخَافُ اللَّهَ ۚ وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٤٨﴾ ع

49. (Kumbukeni) waliposema wanafiki na wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao (yaani wasiokuwa na itikadi nzuri katika Uislamu wao): "Watu hawa (Waislamu) dini yao imewadanganya (hata wanajasirisha leo kukutana na nyinyi)." Na mwenye kutegemea kwa Mwenyezi Mungu (atashinda kwani) kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye ashindaye (na) Mwenye hikima.

إِذْ يَقُولُ الْمُنَٰفِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ
غَرَّ هَٰٓؤُلَآءِ دِينُهُمْ ۗ وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ
فَإِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٩﴾

50. Na laiti ungaliona Malaika wanapowafisha wale waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao na (kuwaambia): Ionjeni adhabu ya moto."

وَلَوْ تَرَىٰٓ إِذْ يَتَوَفَّى الَّذِينَ كَفَرُوا الْمَلَٰٓئِكَةُ
يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَٰرَهُمْ وَذُوقُوا
عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٥٠﴾

51. "Hayo ni kwa sababu ya (maasi) yale yaliyofanywa na mikono yenu. Na hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja (wake)."

ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ
بِظَلَّٰمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٥١﴾

---

Maqureshi wakafurahi wakaona wamepata fursa nzuri ya kumsagasaga Mtume na watu wake. Basi wakatoka wamezatiti barabara—si kama alivyotoka Mtume na wale Masahaba zake.

Mtume na wale watu wake hawakuwa na habari ya kuwa msafara umewapita, na kuwa jeshi kubwa la Maqureshi linawajia kwa vita na kuwa limekwishawakabili. Mpaka wako mbali na Madina ndipowalipopata habari hiyo.

Ukatokea mzozano baina yao Masahaba wenyewe kwa wenyewe. Hawa wanasema walikimbie jeshi la Maqureshi, waufuatie msafara, kwani huo wana yakini wataushinda, na hawana yakini hata chembe ya kulishinda jeshi la Maqureshi, wasitafute kusagwasagwa bure.

Lakini kwa bahati walikutana kwa ghafla tu—hilo jeshi la Maqureshi la vita na jeshi la Waislamu. Ule msafara ukawa uko mbali na wote. Basi huu ndio muradi wa Aya ya 42.

43. Mtume alioteshwa usiku namna hivi, akawahadithia Masahaba.

45. Hapana jambo linalomuezesha mtu kupata analotaka kama kustahamili katika kutaka kulipata alitakalo mpaka alipate. 'Mstahamilivu hula mbivu.' Ama mwenye haraka akiona halipati hilo jambo, huliwachilia mbali; akalikosa. Kazi ya bure imepita.

46. Na katika jambo baya kabisa linalowaharibia watu mambo yao ni kutostahamiliana. Ikawa kupanda mori na kuogmbana na kutawanyika; na yao yakavunjika.

48. Inasemekana kuwa Maqureshi kabla ya kuondoka na jeshi lao kwenda kukabiliana na Mtume, walitaakhari kidogo, wakiwaza namna ya kuilinda nchi yao ya Makka na maadui zao wa kabila ya Bani Kinana. Waliogopa wasije wakatoka na jeshi lao lote hilo kwenda kumpiga Mtume, na huku nyuma wakaja maadui zao kuwashambulia wake zao na mama zao na watoto wao na mali yao na kila kilicho chao.

Basi mara aliwatokea Iblisi kwa sura ya raisi wa ile kabila iliyo adui sana nao. Nayo ni kabila ya Bani Kinana, akawaambia maneno hayo yaliyomo katika Aya hii ya 48 kuwa wasiwe na khofu ya kushambuliwa na kabila yake ya Kibani Kinana. Yeye atawazuilia kushambuliwa nyuma yao. Basi akawapa ahadi kwa hayo mpaka wakamsadiki, wakatoka kwenda kupigana na Nabii Muhammad, na hali ya kuwa nyoyo zao zimetua kuwa hawatashambuliwa. Na yeye akawafuata kwenda huko; akawa pamoja nao hata wakati wa kupigana. Viliposhtadi vita, akaona Malaika wameshuka, alikimbia. Yeye aliweza kuwaona kwa kuwa si Binadamu.

Tena—katika kukataa kwao miujiza na visivyoonekana — wameandika hivi: *"Shetani alipowapambia vitendo*

52. (Hali yao hawa) ni kama hali ya watu wa Firauni na wale waliokuwa kabla yao: walizikataa Aya za Mwenyezi Mungu, kwa hivyo Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa sababu ya yale makosa yao. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, na Mkali wa kuadhibu.

كَدَأْبِ آلِ فِرْعَوْنَ ۙ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٢﴾

53. Hayo (ya kuwafika balaa hizi) ni kwa sababu Mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu, hata wabadilishe wao yaliyomo nyoyoni mwao (wende nyendo mbaya ndipo Mwenyezi Mungu awaondoshee neema yao). Na hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia (kila jambo) na ni Mwenye kulijua

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّرًا نِّعْمَةً أَنْعَمَهَا عَلَىٰ قَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ ۙ وَأَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٥٣﴾

54. (Hali yao hao) ni kama hali ya watu wa Firauni na wale waliokuwa kabla yao; walizikadhibisha Aya za Mola wao, kwa hivyo tukawaangamiza kwa sababu ya madhambi yao, na tukawazamisha watu wa Firauni. Na wote walikuwa madhalimu.

كَدَأْبِ آلِ فِرْعَوْنَ ۙ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ كَذَّبُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُم بِذُنُوبِهِمْ وَأَغْرَقْنَا آلَ فِرْعَوْنَ ۚ وَكُلٌّ كَانُوا ظَالِمِينَ ﴿٥٤﴾

55. Nyama walio waovu kabisa (yaani watu waovu kabisa) mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaokufuru (kwa inadi tu, japo wanajua kuwa hayo yao siyo ya haki). Basi hawataamini.

إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِندَ اللَّهِ الَّذِينَ كَفَرُوا فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٥﴾

56. Ambao umepeana nao ahadi, kisha wanavunja ahadi yao kila mara, wala hawaogopi.

الَّذِينَ عَاهَدتَّ مِنْهُمْ ثُمَّ يَنقُضُونَ عَهْدَهُمْ فِي كُلِّ مَرَّةٍ وَهُمْ لَا يَتَّقُونَ ﴿٥٦﴾

57. Basi ukiwakuta vitani (pigana nao hata) uwakimbize (kwa adabu utakayowatia hawa) walio nyuma yao ili wapate kufahamu (kuwa mambo hayo yatawaletea mabaya).

فَإِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِم مَّنْ خَلْفَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٥٧﴾

58. Na kama ukiogopa khiana kwa watu (mliofanya nao ahadi) basi watupie (ahadi yao) kwa usawa; hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wafanyao khiana.

وَإِمَّا تَخَافَنَّ مِن قَوْمٍ خِيَانَةً فَانبِذْ إِلَيْهِمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِنِينَ ﴿٥٨﴾

---

*vyao.* Hapa Shetani mradi wake ni mtu . . ." Hakuna mfasiri hata mmoja aliyesema hivi, hata huyo mwenye *Ruhul Maany* katika kuifasiri Aya hii katika sahifa ya 14 ya Juzuu ya 10; na wengineo, ambao wamejidai kuwataja mwanzo wa tafsiri yao. Wote wamesema kuwa Shetani aliwazainishia katika (a) nyoyo zao tu haya na aliwadhihirikia khasa kwa (b) kujisawirisha kwa sura ya Suraqa bin Malik. Siyo Suraqa mwenyewe amewaambia haya, kama walivyoonyesha wao. Basi maneno yao hayo ni uwongo.

49. Jiweke tayari barabara kumkabili adui, kisha umtegemee Mwenyezi Mungu.

51. Na Roho za Makafiri zinapotolewa hutolewa kwa taabu kubwa kabisa; lakini wanaokuwa hapo hawaoni, kwa kuwa sisi hatuzioni roho na mambo yaliyokhusika na roho. Sisi huona kiwiliwili cha mwenye kufa. Tukaona wengine wanakufa kwa taabu na wengine wanakufa kwa taratibu. Basi taabu ile tunayoiona kwa wale wanaokufa kwa taabu, ni taabu ya kiwiliwili, sio hiyo taabu ya roho wanayoipata makafiri. Hii taabu ya kiwiliwili inakhusiana na nguvu za huyo maiti, haikhusu wema wake wala ubaya wake. Utawaona wabaya wengi wamekufa taratibu, na wema wengi waliokufa kwa taabu. Basi taabu hiyo ni ya kiwiliwili tu kwa kuwa walikuwa wana nguvu, hawajatopewa na maradhi. Siyo hiyo taabu inayopata roho. Basi tusishituke tukiona watu wema wamekufa kwa taabu, na watu wabaya wamekufa kwa taratibu. Haya ni maonekano ya kiwiliwili, nayo yamekhusiana na nguvu za

59. Wala wale waliokufuru wasifikiri kwamba wao wamekwishatangulia (mbele, Mungu hawapati); la, wao hawatamshinda (Mwenyezi Mungu).

60. Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu mziwezao (silaha), na mafarasi yaliyofungwa (kufuga), tayari tayari (mipakani). ili kwazo (nguvu hizi) muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, (mnaowajua) na pia (maadui zenu) wengineo wasiokuwa wao, msiowajua nyinyi (lakini) Mwenyezi Mungu anawajua. Na chochote mtakachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu (kama hii misaada ya vita vya Jihadi) mtarudishiwa kamili sawasawa wala hamtadhulumiwa.

61. Na kama (hao maadui) wakielekea katika amani, nawe pia ielekee na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika yeye ndiye asikiaye (na) ajuaye.

62. Na kama wakitaka kukukhadaa basi Mwenyezi Mungu atakutoshelezea. Yeye ndiye aliyekusaidia kwa nusura yake na kwa waliokuamini.

63. Na akaziunga nyoyo zao (wakapendana wote hao Masahaba zako); hata kama ungalitoa vyote vilivyomo ardhini usingaliweza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaunganisha. Hakika Yeye ni Mbora na Mwenye hikima.

64. Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na wale waliokufuata katika hao walioamini. (Atakutoshelezeeni maadui zenu, atakukifieni).

65. Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Wahimize walioamini wende vitani. Wakipatikana kwenu watu ishirini wanaosubiri watashinda mia mbili (katika hao makafiri. Basi nyinyi mkiwa ishirini lazima msimame mupigane na watu miteni). Na kama wakiwa watu mia moja kwenu watashinda elfu moja ya wale waliokufuru, maana hao ni watu wasiofahamu (uhai wa Akhera, basi wanaogopa kupigana kwa ushujaa sana wasije wakafa. Basi watu mia katika nyinyi wasiwakimbie watu elfu katika wao).

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَبَقُوا ۚ إِنَّهُمْ لَا يُعْجِزُونَ ﴿٥٩﴾

وَأَعِدُّوا لَهُم مَّا اسْتَطَعْتُم مِّن قُوَّةٍ وَمِن رِّبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَآخَرِينَ مِن دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ ۚ وَمَا تُنفِقُوا مِن شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٦٠﴾

وَإِن جَنَحُوا لِلسَّلْمِ فَاجْنَحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۚ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦١﴾

وَإِن يُرِيدُوا أَن يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ اللَّهُ ۚ هُوَ الَّذِي أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾

وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ ۚ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مَّا أَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٣﴾

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٤﴾ ع

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ ۚ إِن يَكُن مِّنكُمْ عِشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ ۚ وَإِن يَكُن مِّنكُم مِّائَةٌ يَغْلِبُوا أَلْفًا مِّنَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَفْقَهُونَ ﴿٦٥﴾

---

kiwiliwili na udhaifu wake tu.

53. Mwenyezi Mungu hawabadilishii viumbe vyake neema alizowapa mpaka wabadilishe wao mwendo.

56. Nguvu za Mtume zilipokuwa kubwa baada ya kukaa Madina, Waarabu wengine makafiri waliandikiana naye mikataba kuwa wao hawatampiga Mtume, na Mtume asiwapige wao. Basi Mtume alikamata barabara ahadi yake; hakupata kuvunja hata mara moja. Lakini baadhi ya wale Waarabu makafiri walikuwa waongo; wakipata fursa huja wakampiga Mtume.

Basi Mtume anaambiwa hapa katika Aya ya 57 kuwa yakitokea haya na akasimama mtume kupigana nao, basi naawatie adabu kali kabisa hata waogope wale waitifaki wengine kufanya Uitifaki wa unafiki kwa kuchelea yasije

الْآنَ خَفَّفَ اللَّهُ عَنكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفًا ۚ
فَإِن يَكُن مِّنكُم مِّائَةٌ صَابِرَةٌ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ ۚ
وَإِن يَكُن مِّنكُمْ أَلْفٌ يَغْلِبُوا أَلْفَيْنِ بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ
وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٦٦﴾

66. Sasa Mwenyezi Mungu amekukhafifishieni, maana anajua ya kwamba kuna udhaifu (sasa) kwenu (kwa kuwa vita vimeendelea kwa muda mrefu). Kwa hivyo wakiwa watu mia moja kwenu wenye subira nawawashinde watu mia mbili kwao; na kama wakiwa elfu moja miongoni mwenu nawawashinde elfu mbili; kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri. (Yaani sasa wanaambiwa kila Mwislamu mmoja akabiliane na makafiri wawili).

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَن يَكُونَ لَهُ أَسْرَىٰ حَتَّىٰ
يُثْخِنَ فِي الْأَرْضِ ۚ تُرِيدُونَ عَرَضَ الدُّنْيَا
وَاللَّهُ يُرِيدُ الْآخِرَةَ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٧﴾

67. Haimpasii Nabii kuwa na mateka mpaka apigane (sana) na kushinda (barabara) katika nchi (ndipo achukue mateka). Mnataka vitu vya dunia, hali Mwenyezi Mungu anataka (mpate thawabu za) Akhera! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, (na) Mwenye hikima.

لَّوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيمَا أَخَذْتُمْ
عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٦٨﴾

68. Isingalikuwa hukumu iliyotangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu (kuwa mwenye kujitahidi mwisho wa jitihada yake hateswi), bila shaka ingalikupateni adhabu kubwa kwa yale mliyoyachukua.

فَكُلُوا مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلَالًا طَيِّبًا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ
إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٩﴾

69. Basi kuleni katika vile mlivyoteka (vitani), ni halali (yenu sasa) na vizuri, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُل لِّمَن فِي أَيْدِيكُم مِّنَ الْأَسْرَىٰ إِن يَعْلَمِ
اللَّهُ فِي قُلُوبِكُمْ خَيْرًا يُؤْتِكُمْ خَيْرًا مِّمَّا أُخِذَ مِنكُمْ
وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٠﴾

70. Ewe Mtume (wa Mwenyezi Mungu)! Waambie wale mateka waliomo mikononi mwenu: "Kama Mwenyezi Mungu akiona wema wo wote nyoyoni mwenu (mkasilimu) basi atakupeni vizuri kuliko vilivyochukuliwa kwenu na atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu."

---

yakawapata haya yaliyowapata wenzao wanafiki. Ama kwenda kuwapiga watu bure bure, haya hayamo katika Uislamu.

58. Hapa anaambiwa Mtume kwamba akiona kwa waitifaki wake makafiri alama za kuwa watamfanyia khiana wampige, basi yeye asiwafanyie khiana akapigana nao pasina kuwajuvya. Basi naawajuvye mbele kuwa "Mimi nakuoneni nyinyi mnataka kunipitishia khadaa, basi natuvunje ule mkataba wetu, iwe kila mmoja katika sisi anamuogopa mwenziwe, hamuamini tena." Unaona Uislamu hivi usivyowatakia watu madhara wala usivyojitakia madhara pia. Ishi, na mimi niishi. Huu ndio Uislamu.

63. Kabla ya Uislamu kabila mbili hizi za Madina—Ausi na Khazraji—zikichukiana kweli kweli; hazipaliani moto; muda wa miaka mia na ishirini zimo katika kupigana, ingawa kabila mbili zote hizo ni za ukoo mmoja. Lakini kwa chokochoko za Mayahudi zilikuwa katika hali za kupigana na kuogopana daima pasi na kupendana hata chembe hivi kidogo.

Lakini kwa bahati nzuri zote mbili zilisilimu mara moja, zikawa pamoja na Mtume kuupigania Uislamu wote pamoja mkono mmoja. Wakageuka wakapendana kweli kweli kama kwamba sio wale waliokuwa kama paka na chui.

65. Wanaambiwa Waislamu ikipasa kupigana—wawe na nyoyo ngumu kabisa, aweze Muislamu mmoja kukabiliana na kupigana na watu kumi.

71. Na kama wanataka kukufanyia khiana (haitakudhuru khiyana yao); wao walikwishamfanyia Mwenyezi Mungu khiyana kabla ya hapa (kwa ukafiri wao na kutengua kwao ahadi), lakini akakupa kuwashinda. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

وَإِنْ يُرِيدُوا خِيَانَتَكَ فَقَدْ خَانُوا اللَّهَ مِنْ
قَبْلُ فَأَمْكَنَ مِنْهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ
حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

72. Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao; (Nao ni wale Muhajiri—Waislamu wa Makka) Na wale waliowapa (Muhajiri) mahala pa kukaa (Nao ni Ansari) na wakainusuru (dini ya Mungu); hao ndio marafiki, wao kwa wao (katika kurithiana na mengineyo). Na wale walioamini, lakini hawakuhama, nyinyi hamna haki ya kurithiana nao (wala ya mengineyo) hata kidogo mpaka wahame katika nchi ya kikafiri waje wakae nchi moja na nyinyi). Lakini wakiomba msaada kwenu katika dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipokuwa juu ya watu ambao kuna mapatano baina yenu na wao, (hapo msiwasaidie wao mkapigana na waitifaki wenu, Lakini jitahidini kupatanisha). Na Mwenyezi Mungu anayaona (yote) mnayoyatenda.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا
بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
وَالَّذِينَ آوَوْا وَنَصَرُوا أُولَٰئِكَ
بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ
يُهَاجِرُوا مَا لَكُمْ مِنْ وَلَايَتِهِمْ مِنْ شَيْءٍ
حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا ۚ وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ
فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ إِلَّا عَلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ
وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٧٢﴾

73. Na wale waliokufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipofanya hivi itakuwako chokochoko katika ardhi na maharibiko makubwa.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ إِلَّا
تَفْعَلُوهُ تَكُنْ فِتْنَةٌ فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٧٣﴾

74. Na walioamini wakahama (kuja Madina) na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu (Nao ni Muhajiri); na wale waliowapa (Muhajiri) mahala pakukaa na wakainusuru (dini ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake). (Nao ni Ansari). Hao ndio Waislamu wa kweli. Watapata msamaha (wa Mwenyezi Mungu) na kuruzukiwa kuzuri (kabisa huko Akhera).

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي
سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ آوَوْا وَنَصَرُوا أُولَٰئِكَ
هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا ۚ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٧٤﴾

75. Na wale watakaoamini baadaye (baada ya Muhajiri na Ansari) wakahajiri nao (wakaja Madina kukaa na Mtume na Waislamu wenzao ili wawemkono mmoja kuipigania dini) wakapigana pamoja na nyinyi (katika kupigania dini); basi hao ni katika nyinyi. Na ndugu wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe (katika kurithiana. Ndiyo ilivyo) katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

وَالَّذِينَ آمَنُوا مِنْ بَعْدُ وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا مَعَكُمْ
فَأُولَٰئِكَ مِنْكُمْ ۚ وَأُولُو الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ
بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧٥﴾

67. Siku ya vita vya Badri Waislamu waliwateka mateka sabiini wa kikafiri; wakafanya mkutano Waislamu juu ya habari ya hawa mateka. Masahaba wengine, kama Sayyidna Umar bin Al Khattab—walisema wauawe mateka wote hao kwani ndio katika wale makafiri wakubwa wenye inadiwaliowadhuru Waislamu na kutaka kuuondosha Uislamu. Ama Masahaba wengi kabisa—na miongoni mwao ni Sayyidna Abubakr—wao waliona shauri nzuri ni kuwatoza vikomboleo na kuwaachia kurejea kwao bila ya kufanywa lolote. Basi Mtume akafuata rai hii. Ikaja Aya

hii ya 67 kutaja kuwa hilo silo shauri zuri, maadamu Waislamu hawajachuma nguvu bado. Bora kuwaua maadui makatili nao; ili shina la ukatili lisukuke lianguke.

68. Aya hii inawaondoshea jukumu, kwa kuwa hawakuambiwa mbele kuwa wasifanye hivyo. Na wao wamejitahidi mwisho wa jitihada yao. Na mwenye kujitahidi mwisho wa jitihada yake, akasibu, hupata thawabu mbili—thawabu za (a) Kujitahidi na thawabu za (b) Kusibu. Na mwenye kujitahidi mwisho wa jitihada yake, akakosa, hupewa 7thawabu ya (a) Kujitahidi kwake; na hateswi kwa kule kukosa kwake; ila hujulishwa tu kuwa hayo ni makosa asiyafanye tena.

Tazama Uislamu namna unavyohimiza watu wake kusoma na kujitahidi kutumia akili zao.

70. Mateka wengine walilalamika sana kwa kule kuambiwa wajikomboe kwa kikomboleo ambacho kilikuwa kikubwa, si haba. Basi wanaambiwa hapa kuwa wakisilimu Mwenyezi Mungu atawafungulia milango ya kheri.

72. Wanahimizwa Waislamu wawe wamoja, wawe pamoja. Hapana kitu kama Umoja. Umehimizwa kweli kweli na wametahadharishwa vibaya kabisa wanaovunja umoja.

73. Unatajwa ubaya wa kuwa wamoja na wasiokuwa Waislamu hata wakiwa jamaa. Ujamaa uwe wa Uislamu sio wa Utaifa na Ukabila.

75. Walipohama Waislamu kutoka Makka kuja Madina walipangwa udugu — kila Muhajiri mmoja awe ndugu wa Ansari mmoja, warithiane, wafanyiane kama kila ndugu anavyofanyiana na nduguye—kwa kuwa wale Muhajiri umekatika uungamano wao na ndugu zao walio makafiri huko Makka, wakawa hawapaliani moto—kila mmoja tayari kumtoa roho mwenziwe. Basi ndio wakatafutiwa udugu huu wa dini baina yao na Ansari. Ukawa wa kurithiana na mengineyo. Ikadumu hali hii mpaka mwisho wa mwaka wa nane wa Al Hijra, wakati ambao Makka yote ilisilimu na nchi nyingi za Hijazi, wakawa wale ndugu wa Kimuhajiri wamekutana sasa katika dini moja na wale ndugu zao wa nasaba. Basi kukarejeshwa kurithiana kwa nasaba pamoja na dini, si kurithiana kwa dini moja tu pasi na nasaba au kwa nasaba tu pasi na dini. Kwani yote mawili inataka yasitupwe—udugu wa dini na udugu wa nasaba. Ukipatikana mmojawapo tu, basi utiwe nguvu wa dini kuliko wa nasaba. Lakini zikipatikana upande mmoja zote hizo namna mbili za udugu, basi utakuwa na nguvu upande huo.

آياتها ١٢٩ (٩) سُورَةُ التَّوْبَةِ مَدَنِيَّةٌ (١١٣) ركوعاتها ١٦

*Ina Aya 129* **SURATUT TAWBA** *Ina Makaru 16*

*(Imeteremka Madina)*

1. (Hili ni) tangazo la kujitoa katika dhima (ahadi), litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina.

بَرَآءَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ عَاهَدتُّم مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ①

2. (Waambieni): "Basi tembeeni katika nchi miezi minne (kwa salama, kisha vitakuwa vita baina yenu na sisi); na jueni kwamba nyinyi hamuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na kwamba Mungu ndiye Mwenye kuwadhalilisha makafiri."

فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَأَنَّ اللَّهَ مُخْزِي الْكَافِرِينَ ②

3. Na ni tangazo litokalo kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kujuvywa watu siku ya Hija kubwa ya kwamba Mwenyezi Mungu yu mbali na washirikina; na pia Mtume wake (yu mbali nao; hawana haja na ahadi zao). Basi kama mkitubu ndiyo kheri kwenu, na kama mkikengeuka, basi jueni kwamba nyinyi hamuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu. Na wapashe waliokufuru habari ya adhabu iumizayo (inayowangoja)

وَأَذَانٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى النَّاسِ يَوْمَ الْحَجِّ الْأَكْبَرِ أَنَّ اللَّهَ بَرِيءٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ فَإِن تُبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَبَشِّرِ الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ③

4. Isipokuwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa hao washirikina, kisha hawakukupunguzieni cho chote wala hawakumsaidia yoyote juu yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda wao. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaomuogopa.

إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدتُّم مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ يَنقُصُوكُمْ شَيْئًا وَلَمْ يُظَاهِرُوا عَلَيْكُمْ أَحَدًا فَأَتِمُّوا إِلَيْهِمْ عَهْدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ④

---

1. Hii *Suratut Tawba* haikuanzwa kwa *Bismillahi* kama zilivyoanzwa Sura nyingine. NA SABABU YAKE NI KUWA Sura hii imekuja kutaja mambo yaliyokhusiana na vita, na kuvunja mikataba; mambo ambayo hayapendwi na Uislamu; ila ni kukosa budi tu.

2. Mtume alijitahidi kila namna kuishi vizuri na makafiri; hata akaandikiana nao mikataba ya kutopigana baina yao wala baina ya waitifaki wa kila mmoja katika wao. Lakini baada ya muda mfupi wengi katika makafiri wale walifanya khiana. Walikuja kumpiga Mtume kwa ghafla na wakawapiga waitifaki wake Mtume pia kwa ghafla.

Basi Mwenyezi Mungu akateremsha Sura hii kuvunja mikataba hiyo; usiweko tena mkataba wowote baina yao na Mtume ila kwa wale waliotimiza ahadi.

3. Walijuvywa makafiri habari hii Siku ya Arafa na ya Sikukuu ya mwaka wa 9 wa *Al Hijra*. Mtume alimpeleka Sayyidna Ali Makka akakutane na makafiri wa kila kabila watakaokutana hapo, awape habari hii ya kuwa (a) Wale waliokuwa na mkataba na Mtume — na wasiutimize vilivyo — basi wanapewa muda wa miezi minne tangu siku hiyo ya Arafa. Ikisha miezi minne hapana tena ule mkataba baina yao, kama ilivyo katika Aya ya 5.

Ama wale walioandikiana mkataba na Mtume — na wakauchunga vizuri — hao wataendeshewa mkataba wao mpaka muda wake wishe, kama ilivyobainishwa katika Aya ya 4 ya Sura hii.

5. Makadiyani wamekosea miezi inayoitwa *L-ashhurul Hurum*. Badala ya *Shawwal* inataka atie Mfunguo nne. Wala si kweli maneno yao haya: ". . . makafiri walipewa muda wa miezi minne kuizunguka Bara Arabu yote ili wajionee wenyewe mafanikio yaliyobashiriwa na Uislamu yametimia namna gani." Kwani wakati huo ndio

5. Na ile miezi mitukufu itakapokwisha (Ile miezi minne waliyopewa), basi waueni (piganeni na) washirikina popote muwakutapo, na wakamateni mateka (kama wanavyokufanyieni) na wazungukeni na wakalieni katika kila njia. Lakini wakitubu na wakasimamisha Sala na wakatoa Zaka, basi iacheni njia yao (waacheni). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

6. Na kama mmoja wa washirikina akikuomba umlinde (ili asikie maneno ya Mwenyezi Mungu), basi mlinde asikie maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha (akitoyakubali usimlazimishe wala usimdhuru, bali) mfikishe mahala pake pa amani (kama hataki kufuata Uislamu); Na haya ni kwa ajili ya kuwa hao ni watu wasiojua.

7. Itakuwaje kuwapo ahadi na washirikina mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Mtume wake isipokuwa wale mlioahidiana nao mbele ya Msikiti mtukufu (Al Kaaba, na wakatekeleza ahadi zao)? Basi maadamu wanakunyokeeni kwa uzuri, nanyi pia wanyokeeni kwa uzuri, hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaomuogopa.

8. (Mtatekeleza nyinyi tu ahadi peke yenu) Vipi? Hali wakikushindeni hawatazami kwenu udugu wala ahadi. Wanakufurahisheni kwa vinywa vyao tu, hali nyoyo zao zinakataa (hayo). Na wengi katika wao ni maasi.

9. Wamekhitari thamani ndogo (ya kidunia) kuliko kufuata Aya za Mwenyezi Mungu, na wanazuilia (watu) na njia yake (Mwenyezi Mungu). Hakika ni mabaya kabisa waliyokuwa wakiyafanya.

10. Hawaangalii kwa Muislamu udugu wala ahadi; basi hao ndio wapitao mipaka.

11. Kama wakitubu na wakasimamisha Sala na wakatoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika dini. Na tunazieleza Aya (vizuri) kwa watu wanaojua.

فَإِذَا انْسَلَخَ الْأَشْهُرُ الْحُرُمُ فَاقْتُلُوا
الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ وَخُذُوهُمْ
وَاحْصُرُوهُمْ وَاقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصَدٍ ۚ فَإِنْ تَابُوا
وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا
سَبِيلَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥﴾
وَإِنْ أَحَدٌ مِنَ الْمُشْرِكِينَ اسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ
حَتَّىٰ يَسْمَعَ كَلَامَ اللَّهِ ثُمَّ أَبْلِغْهُ مَأْمَنَهُ ۚ ذَٰلِكَ
بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦﴾
كَيْفَ يَكُونُ لِلْمُشْرِكِينَ عَهْدٌ عِنْدَ اللَّهِ
وَعِنْدَ رَسُولِهِ إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ عِنْدَ
الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۖ فَمَا اسْتَقَامُوا
لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا لَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧﴾
كَيْفَ وَإِنْ يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ لَا يَرْقُبُوا فِيكُمْ
إِلًّا وَلَا ذِمَّةً ۚ يُرْضُونَكُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ وَتَأْبَىٰ
قُلُوبُهُمْ وَأَكْثَرُهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٨﴾
اشْتَرَوْا بِآيَاتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا فَصَدُّوا عَنْ
سَبِيلِهِ ۚ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩﴾
لَا يَرْقُبُونَ فِي مُؤْمِنٍ إِلًّا وَلَا ذِمَّةً ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ
الْمُعْتَدُونَ ﴿١٠﴾
فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ
فِي الدِّينِ ۗ وَنُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

---

kwanza Bara Arabu inaanza kusilimu, waone mafanikio gani?

Tazama Uislamu unavyowapa wasiokuwa Waislamu haki ya kufuata dini waitakayo na kuwahami khasa, wasidhuriwe. Dini gani nyingine inayofanya hivi? Na juu ya hivi maadui wake wanatangaza kuwa Uislamu umesimama kwa upanga. Lakini 'akutukanaye hakuchagulii Tusi.'

10. Ukiwaachia tu wabaya wakufanye watakavyo utaangamia. Mtende anayekutenda, Mche asiyekutenda. Na mara nyingi samehe ikiwa haitakuwa madhara kwako wala kwa Uma.

12. Wamefasiri uwongo waliposema: "Neno *ta'ana* lililotumika hapa maana yake ni *kuchoma kwa mkuki.*" Uwongo. *Ta'ana* hapa ni kutukana, kama ilivyo katika tafsiri zote, kama katika sahifa 32 ya Juzuu ya 10 ya hiyo *Ruuhul Maany* wanayojidai kuitaja kila mara. Huko kuchomana kwa vita kumekwishaingia katika tamko la mwanzo — *Wainnakathuu* . . . Wanataka tu kutia farumu katika hiyo tafsiri yao au taghyiri (mgeuzo) yao

12. Na kama wakivunja viapo vyao baada ya kuahidi kwao na wakatukana dini yenu, basi waueni (piganeni nao) waongozi wa ukafiri. Hakika viapo vyao havina maana; (Piganeni nao) ili wapate kujizuia (na kufanya ubaya huo).

وَإِن نَّكَثُوٓا أَيْمَٰنَهُم مِّنۢ بَعْدِ عَهْدِهِمْ
وَطَعَنُوا فِى دِينِكُمْ فَقَٰتِلُوٓا أَئِمَّةَ ٱلْكُفْرِ
إِنَّهُمْ لَآ أَيْمَٰنَ لَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَنتَهُونَ ﴿١٢﴾

13. Je, hamtapigana na watu waliovunja ahadi zao na wakafunga nia ya kumfukuza Mtume, nao ndio (pia) waliokuanzeni mara ya kwanza? Je, mnawaogopa? Basi Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi mumuogope; ikiwa nyinyi mumeamini.

أَلَا تُقَٰتِلُونَ قَوْمًا نَّكَثُوٓا أَيْمَٰنَهُمْ وَهَمُّوا بِإِخْرَاجِ
ٱلرَّسُولِ وَهُم بَدَءُوكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ أَتَخْشَوْنَهُمْ
فَٱللَّهُ أَحَقُّ أَن تَخْشَوْهُ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾

14. Piganeni nao, Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa mikono yenu, na awafedheheshe na akunusuruni juu yao, na avipoze vifua vya Waislamu (vifurahi).

قَٰتِلُوهُمْ يُعَذِّبْهُمُ ٱللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْزِهِمْ وَ
يَنصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُّؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾

15. Na aondoe joto la ghadhabu lililokuwa katika nyoyo zao (Waislamu); na Mwenyezi Mungu humwelekea kwa rehema amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

وَيُذْهِبْ غَيْظَ قُلُوبِهِمْ ۗ وَيَتُوبُ ٱللَّهُ عَلَىٰ
مَن يَشَآءُ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٥﴾

16. Je, mnadhani kuwa mtaachwa, na hali Mwenyezi Mungu hakuwabainisha wale waliopigania dini miongoni mwenu na wasiwafanye rafiki wa moyo isipokuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waislamu (wenzao)? Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyafanya.

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تُتْرَكُوا وَلَمَّا يَعْلَمِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ
جَٰهَدُوا مِنكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوا مِن دُونِ ٱللَّهِ وَلَا
رَسُولِهِۦ وَلَا ٱلْمُؤْمِنِينَ وَلِيجَةً ۚ وَٱللَّهُ خَبِيرٌۢ بِمَا
تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾ ع

17. Haiwi kwa washirikina (kuhisabika) wanaamirisha Miskiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudia kwa ukafiri. Hao (ndio ambao) vitendo vyao vyema vimeruka patupu, na katika Moto watakaa daima.

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَن يَعْمُرُوا مَسَٰجِدَ ٱللَّهِ
شَٰهِدِينَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِم بِٱلْكُفْرِ ۚ أُولَٰٓئِكَ حَبِطَتْ
أَعْمَٰلُهُمْ وَفِى ٱلنَّارِ هُمْ خَٰلِدُونَ ﴿١٧﴾

18. Wanaoamirisha Miskiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na kusimamisha Sala na kutoa Zaka na hawamuogopi yoyote ila Mwenyezi Mungu; basi hao ndio wanaotarajiwa kuwa miongoni mwa walioongoka.

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسَٰجِدَ ٱللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ
وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا ٱللَّهَ
فَعَسَىٰٓ أُولَٰٓئِكَ أَن يَكُونُوا مِنَ ٱلْمُهْتَدِينَ ﴿١٨﴾

19. Je, mnafanya kuwanywesha maji mahujaji na kuuamirisha Msikiti Mtukufu ni sawa na (kazi ya)

أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ ٱلْحَآجِّ وَعِمَارَةَ ٱلْمَسْجِدِ

---

16. Inakuja kwa Waislamu misukosuko na vita ili wabainike wapi Waislamu wa kweli na wapi wanafiki wanaojidai kuwa Waislamu, kumbe waongo. Basi misiba mengine ni maslaha kutufika, ndiyo maana Mwenyezi Mungu akafanya itufike.

17. Masahaba walipohama Makka wakenda Madina, makafiri waliokuwa Makka walikuwa wanaishughulikia *Al Kaaba* kwa kuitengeneza na mengineyo. Basi wakawa wanajisifu kuwa wao wanaamirisha Msikiti wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiyo anawaambia kuwa hawahisabiki kuwa wanaamirisha msikiti wa Mwenyezi Mungu maadamu wanaacha kumuabudu yeye wakaabudu masanamu, na vile vile maadamu wanamuabudu yeye pamoja na masanamu na maadamu hawayafuati mengine yote yaliyoamrishwa na Uislamu. Basi kushughulikia misikiti siyo amali bora tu.

*Kuamirisha* ni kusimamisha jambo ili litengenee.

19. Tangu zama za ukafiri Maqureshi walikuwa wakiwatengenezea mahodhi ya maji watu wanaokuja kuhiji na wakiwatengenezea chakula cha bure wale mahujaji waliokuwa masikini. Basi walijifakharisha kwa haya juu ya

wale walioamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

الْحَرَامِ كَمَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهَدَ
فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۚ لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ لَا
يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾

20. Wale walioamini na wakahama na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na kwa nafsi zao wana cheo kikubwa mbele ya Mwenyezi Mungu; na hao ndio watakaotengenekewa (sio hao wanaoshughulika na hayo wanayoyashughulikia Maqureshi).

الَّذِينَ آمَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي
سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ أَعْظَمُ
دَرَجَةً عِنْدَ اللَّهِ ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

21. Mola wao anawabashiria (anawapa habari njema za) rehema zitokazo kwake, na radhi (zake) na mabustani ambayo humo watapata neema zitakazodumu

يُبَشِّرُهُمْ رَبُّهُمْ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَرِضْوَانٍ وَجَنَّاتٍ
لَهُمْ فِيهَا نَعِيمٌ مُقِيمٌ ﴿٢١﴾

22. Watakaa humo milele. Hakika Mwenyezi Mungu kwake kuna malipo makubwa kabisa.

خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٢﴾

23. Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi (vyenu) ikiwa wanastahabu (wanapenda) ukafiri kuliko Uislamu. Na katika nyinyi atakayewafanya hao kuwa ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا آبَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ
أَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْإِيمَانِ ۚ وَمَنْ
يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾

24. Sema: "Kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda; (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania dini yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi (njia iliyonyooka).

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ
وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ
تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِنُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ
مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّىٰ
يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٤﴾

25. Bila shaka Mwenyezi Mungu amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Huneyni (pia); ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni chochote, na ardhi ikawa dhiki juu yenu; ingawa ilikuwa yenye wasaa, kisha mkageuka mkarudi nyuma (mnakimbia).

لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ ۙ وَيَوْمَ
حُنَيْنٍ ۙ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ
شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ
وَلَّيْتُمْ مُدْبِرِينَ ﴿٢٥﴾

---

Waislamu; na Mwenyezi Mungu akawajibu kwa haya yaliyomo katika Aya hii ya 19.

Basi ndiyo kuna watu wengine wakiwa wamehiji, wanasoma Maulidi, huona ndiyo wamekwisha kufanya mambo ya dini; wala haya hayamo katika *Jihad fy Sabylil Lah.*

Ilipokuja amri ya kuambia Waislamu watoke Makka wakakae Madina, wengine waliona uzito kidogo kufarikiana na wazee wao (waliokuwa makafiri) na watoto wao na wake zao na jamaa zao, na kutupa mali zao na biashara zao walizokuwa wanaendesha huko Makka. Basi wakaambiwa maneno haya yaliyomo katika Aya ya 23 na ya 24.

25. Hakupata Mtume kutoka na jeshi kubwa kabisa kama jeshi alilotoka nalo kwenda kwenye jangwa la Huneyn kukabiliana na makafiri wa nchi ya Taif. Ndiyo mara yake ya awali kutoka na jeshi la watu elfu kumi na mbili.

26. Kisha Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu wake juu ya Mtume wake na juu ya walioamini. Na akateremsha majeshi (ya Malaika) ambayo hamkuyaona, na akawaadhibu wale waliokufuru; na hayo ndiyo malipo ya makafiri.

ثُمَّ اَنْزَلَ اللّٰهُ سَكِيْنَتَهٗ عَلٰى رَسُوْلِهٖ وَعَلَى
الْمُؤْمِنِيْنَ وَاَنْزَلَ جُنُوْدًا لَّمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ
الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ۚ وَذٰلِكَ جَزَآءُ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٢٦﴾

27. Kisha baada ya haya Mwenyezi Mungu atawasamehe awatakao (katika wale makafiri maadamu watasilimu watubie). Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

ثُمَّ يَتُوْبُ اللّٰهُ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ عَلٰى مَنْ يَّشَآءُ ۚ
وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢٧﴾

28. Enyi mlioamini! Hakika washirikina ni najisi, kwa hivyo wasiukaribie huo Msikiti Mtukufu baada ya mwaka wao huu. Na kama mkikhofia umasikini, basi karibuni hivi Mwenyezi Mungu atakutajirisheni kwa fadhila zake akipenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِنَّمَا الْمُشْرِكُوْنَ نَجَسٌ
فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هٰذَا ۚ
وَاِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيْكُمُ اللّٰهُ مِنْ
فَضْلِهٖۤ اِنْ شَآءَ ۚ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٨﴾

29. Piganeni na wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho wala hawaharimishi alivyoviharimisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa wale waliopewa Kitabu; (piganeni nao) mpaka watoe kodi kwa hiari yao, hali wametii.

قَاتِلُوا الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَلَا بِالْيَوْمِ
الْاٰخِرِ وَلَا يُحَرِّمُوْنَ مَا حَرَّمَ اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗ
وَلَا يَدِيْنُوْنَ دِيْنَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ
حَتّٰى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَنْ يَّدٍ وَّهُمْ صٰغِرُوْنَ ﴿٢٩﴾ ع

30. Na Mayahudi wanasema: "Uzeri ni mwana wa Mwenyezi Mungu;" na Wakristo wanasema "Masihi ni mwana wa Mwenyezi Mungu"; haya ndiyo wasemayo kwa vinywa vyao (pasi na

وَقَالَتِ الْيَهُوْدُ عُزَيْرُ اِبْنُ اللّٰهِ
وَقَالَتِ النَّصٰرَى الْمَسِيْحُ ابْنُ اللّٰهِ ۚ ذٰلِكَ قَوْلُهُمْ

---

Basi walipanda kichwa kidogo Masahaba kwa kujiona wengi vile baada ya kuwa watu wachache kabisa. Basi wakasema: "Hatutashindwa leo kwa uchache."

Mwenyezi Mungu asiupende msemo huu. Basi walipokuja kukabiliana kwa ghafla na maadui zao — kabla ya kujiweka tayari — walishambuliwa barabara na maadui zao hao; hata mwisho wake walipoona vimoto tena — walikwenda mbio, wanawakimbia hao maadui; kila mtu Rabi Rabi Nafsi tu. Basi kujiona ni jambo baya kabisa. Na moja ya ubaya wake ni kutokaa kwa hadhari.

Kisha Mtume akawakusanya tena akashambuliana na hao maadui; hapo sasa ndipo waliposhinda.

28. Baada ya Mtume kuiteka Makka ilitolewa ilani kuwa wale makafiri — waliokuwa wakija Makka kuabudu masanamu yao waliyoyaweka huko Makka — hawana ruhusa tena kuja huko Makka kuabudu masanamu hayo. Na masanamu hayo yalivunjiliwa mbali. Mambo yao yalikuwa ya najisi; moja katika hayo walikuwa wakihiji tuputupu.

Baadhi ya watu ilipotolewa ilani hii waliogopa kuharibikiwa nchi ya Makka kwani hao waliozuiliwa kuja walikuwa wakija kibiashara pia; wakileta vya kwao na wakinunua vya Makka. Basi Mwenyezi Mungu anawatuliza nyoyo zao hao waliofazaika kwa haya kuwa wakifunga milango ya shari, Mungu atawafungulia milango ya kheri.

29. Maadamu makafiri wanapigana na Waislamu basi wamepewa ruhusa Waislamu kupigana nao. Na wakiwashinda, wakitaka wenyewe kwa khiari zao kusilimu basi wanaweza kusilimu. Na kama hawataki kusilimu, wanataka kuendelea na dini yao, basi wanaweza kuendelea na dini yao; lakini wataamrishwa kutoa kodi ya kichwa ya kulipwa kila mwaka juu ya kila aliyebaleghe; ili kuonyesha kuwa wao wamo katika taa ya Uislamu; hawana Waislamu hatari upande wao. Na itapasa dola ya Waislamu kuwahami watu hao dhidi ya maadui zao—kuwahami roho zao, viwiliwili vyao, dini yao, dunia yao, mali yao na kila kilicho chao. Na kitoleo hiki huitwa *Jizya*. Nacho ni kitu kidogo sana.

30. Uzeri ni Mtume katika Mitume walioletewa Mayahudi. Badala ya kumuamini kuwa ni Mtume wa

kuyapima). Wanayaiga maneno ya wale walio kufuru kabla yao, Mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gani hawa!

بِأَفْوَاهِهِمْ ۖ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن
قَبْلُ ۚ قَاتَلَهُمُ اللَّهُ ۚ أَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٣٠﴾

31. Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na (wamemfanya) Masihi mwana wa Maryamu (pia Mungu), hali hawakuamrishwa isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo.

اتَّخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن
دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا
لِيَعْبُدُوا إِلَٰهًا وَاحِدًا ۖ لَّا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ سُبْحَانَهُ
عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

32. Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, lakini Mwenyezi Mungu amekataa isipokuwa kuitimiza nuru Yake, ijapokuwa makafiri wanachukia.

يُرِيدُونَ أَن يُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَيَأْبَى
اللَّهُ إِلَّا أَن يُتِمَّ نُورَهُ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٣٢﴾

33. Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili aijaalie kushinda (dini hii) dini zote; ijapokuwa watachukia hao washirikina.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ
لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

34. Enyi mlioamini! Wengi katika makasisi (wanavyuoni wa Mayahudi na Manasara) na watawa (wao) wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Mwenyezi Mungu. Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wape habari za adhabu inayoumiza (inayowangoja).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ
لَيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَيَصُدُّونَ عَن
سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَالَّذِينَ يَكْنِزُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا
يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٤﴾

35. Siku (mali yao) yatakapotiwa moto katika moto wa Jahanamu, na kwa hayo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, (na huku wanaambiwa): "Haya ndiyo (yale mali) mliojilimbikia (mliyojikusanyia) nafsi zenu, basi onjeni (adhabu ya) yale mliyokuwa mkikusanya."

يَوْمَ يُحْمَىٰ عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوَىٰ بِهَا
جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ ۖ هَٰذَا مَا
كَنَزْتُمْ لِأَنفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنتُمْ
تَكْنِزُونَ ﴿٣٥﴾

---

Mwenyezi Mungu walimuitakidi kuwa ni mtoto wa Mwenyezi Mungu kama Manasara na Nabii Isa. Bali takriba umma zote za nyuma — za kabla ya Mayahudi na Manasara — zikiwaitakidia utoto wa Mungu baadhi ya wakubwa wao. Basi Mayahudi na Manasara sio waliopotoka mwanzo katika jambo hili la kuwaitakidia utoto wa Mungu baadhi ya watu wao. Wao imekuwa kama wanaiga tu hayo yaliyosemwa na makafiri walio kuwa kabla yao.

32. Wanajitahidi Mayahudi na Manasara na wenye dini nyingine kuusingizia uwongo Uislamu ili kuuchukizisha mbele ya macho ya viumbe ili wasiufuate. Lakini wapi! Kila siku Uislamu unazidi kufuatwa na watu wa kila jinsi katika kila makontinenti, hata Australia na Greenland.

Katika Aya hii waliyoifanya ya 33 wametia uwongo wao wa kumdaia mtu wao Utume na Unabii Isa. Tumeuvunja ukafiri wa Unabii katika Marejezo ya Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah.* Na tumevunja ukafiri wao wa kumdaia "Unabii Isa" katika Aya ya 115 ya *Suratul Baqarah.*

Na wamejidai tena vile vile kutaja kitabu *Bayani* ili kudhanisha watu kuwa kitabu hicho kimetungwa na asiyekuwa wao. Hicho ni kitabu chao wenyewe cha kutaja Itikadi za dini yao. Wanadhanisha watu kuwa ni kitabu cha Kiislamu. Majambazi kweli kweli. Wanasukuma MIJILO tu, wala hawamjali Mungu. (*Mijilo* = uwongo usiofichikana.)

34. Inabainishwa hapa kuwa kuna watu wa dini wabaya wanaokula mali za watu kwa njia za haramu. Basi

36. Idadi ya mezi (ya mwaka mmoja) mbele ya Mwenyezi Mungu ni mezi kumi na mbili katika ilimu ya Mwenyezi Mungu (Mwenyewe tangu) siku alipoumba mbingu na ardhi. Katika hiyo imo minne iliyo mitukufu kabisa (nayo ni Rajabu, Mfunguo Pili, Mfunguo Tatu, na Mfunguo Nne). (Kufanya) hivi ndiyo dini iliyo sawa. Basi msijidhulumu nafsi zenu (kwa kufanya maasi) katika (mezi) hiyo. Na nyote piganeni na washirikina kama wao wote wanavyopigana nanyi; na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaomuogopa.

إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللّٰهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِي
كِتٰبِ اللّٰهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ مِنْهَا
أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ ۚ ذٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ ۚ فَلَا
تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ ۚ وَقَاتِلُوا
الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقَاتِلُونَكُمْ كَافَّةً ۚ
وَاعْلَمُوا أَنَّ اللّٰهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿٣٦﴾

37. Bila shaka kuakhirisha (Mezi Mitukufu isije upesi) ni kuzidi katika ukafiri; kwa hayo hupotezwa wale waliokufuru; wanauhalalisha (Mwezi mtukufu), mwaka mmoja na kuuharimisha mwaka (mwengine), ili wafanye kuwa sawa idadi ya ile (mezi) aliyoitukuza Mwenyezi Mungu (aliyoiharimisha Mwenyezi Mungu); kwa hivyo huhalalisha alivyoviharimisha Mwenyezi Mungu. Wamepambiwa ubaya wa vitendo vyao (hivi). Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri.

إِنَّمَا النَّسِيءُ زِيَادَةٌ فِي الْكُفْرِ يُضَلُّ بِهِ الَّذِينَ
كَفَرُوا يُحِلُّونَهُ عَامًا وَيُحَرِّمُونَهُ عَامًا لِيُوَاطِئُوا
عِدَّةَ مَا حَرَّمَ اللّٰهُ فَيُحِلُّوا مَا حَرَّمَ اللّٰهُ ۚ زُيِّنَ
لَهُمْ سُوءُ أَعْمَالِهِمْ ۗ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ
الْكٰفِرِينَ ﴿٣٧﴾ ع

38. Enyi mlioamini! Mna nini mnapoambiwa "Nendeni (kupigana) kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu" mnajitia uzito katika ardhi? Je, mumekuwa radhi na maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kwa (mkabala wa maisha ya) Akhera ni kidogo tu.

يٰأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ
انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللّٰهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ ۚ
أَرَضِيتُمْ بِالْحَيٰوةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ ۚ فَمَا مَتَاعُ
الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٣٨﴾

39. Kama hamtakwenda atakuadhibuni kwa adhabu inayoumiza, na atawaleta watu wengine badala yenu, wala hamtamdhuru (Mungu) cho chote (mkitopigania dini yake); na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ۙ وَيَسْتَبْدِلْ
قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئًا ۗ وَاللّٰهُ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٩﴾

---

wataadhibiwa kama watu wengine, sio kuwa itawafutu adhabu kwa kuwa ni Masheikhe au Masharifu (wajukuu wa Mtume); si kweli haya.

36. Kuna mezi mingine mitukufu zaidi kama hii minne na Ramadhani. Basi inataka mtu ajitahidi zaidi mezi hii kufanya mema na kuacha mabaya.

37. Nabii Ibrahimu na Nabii Ismaili waliwafundisha Waarabu kuihishimu sana sana mezi minne hii: Mfunguo pili, Mfunguo tatu, Mfunguo nne na Rajabu; wasifanye jambo lolote baya, khasa kupigana.

Lakini karne nyingi zilipopita waliionea uzito sharti hii ya kutopigana. Basi wakaanza kufanya ujanja kuikimbiakimbia. Wakaanza kuiongeza mezi ya mwaka. Badili ya kuwa mwaka mmoja mezi kumi na mbili wakaifanya mezi kumi na tatu au zaidi ili ikawie kufika ile mezi minne inayokatazwa kupiganwa.

Kwa hivyo kila mwaka wanapokutana Makka siku ya Arafa huondoka wakubwa wakatoa khabari kuwa mwaka huo mpya ujao waufanye mezi kumi na tatu au kumi na nne, kwa kuihisabu mara mbili baadhi ya ile mezi iliyokatazwa kupiganwa. Kama kusema: "Ukiandama Mfunguo nne uliotukabili tuwite mwezi mpya Mfunguo tano wa mwanzo, na wa pili wake tuwite Mfunguo tano wa pili" badala ya kuwita Mfunguo sita. Tena wa tatu ndio wawite Mfunguo sita ili ile mezi minne ikawie kufika. Ndiyo Mwenyezi Mungu anawatukana hapa kuonyesha kuwa japo wanatukuza mezi minne katika mwaka, lakini mezi minne la haiwi thuluthi ya mwaka kwani mwaka

40. Kam hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake, (peke yao); walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake: "Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi." Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayeshinda na ndiye Mwenye hikima.

إِلَّا تَنصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ ٱللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ ٱلَّذِينَ
كَفَرُوا۟ ثَانِىَ ٱثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِى ٱلْغَارِ إِذْ يَقُولُ
لِصَٰحِبِهِۦ لَا تَحْزَنْ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا ۖ فَأَنزَلَ ٱللَّهُ
سَكِينَتَهُۥ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُۥ بِجُنُودٍ لَّمْ تَرَوْهَا وَ
جَعَلَ كَلِمَةَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ٱلسُّفْلَىٰ ۗ وَكَلِمَةُ
ٱللَّهِ هِىَ ٱلْعُلْيَا ۗ وَٱللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾

41. Nendeni (vitani) mkiwa wepesi na mkiwa wazito (wazima au wagonjwa); na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu; mkiwa watu mnaojua (jambo).

ٱنفِرُوا۟ خِفَافًا وَثِقَالًا وَجَٰهِدُوا۟ بِأَمْوَٰلِكُمْ
وَأَنفُسِكُمْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ
إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾

42. Kama ingalikuwa faida iliyo nyepesi (kupatikana) na safari fupi, kwa yakini wangalikufuata (hao wanaojipa Uislamu wa uwongo). Lakini safari hii ya taabu imekuwa ndefu kwao. Nao wataapa kwa Mwenyezi Mungu, "Kama tungaliweza bila shaka tungelitoka pamoja nanyi." Wanaangamiza nafsi zao; na Mwenyezi Mungu anajua (kwa hakika) kuwa hao ni waongo (tu).

لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا وَسَفَرًا قَاصِدًا لَّٱتَّبَعُوكَ
وَلَٰكِنۢ بَعُدَتْ عَلَيْهِمُ ٱلشُّقَّةُ ۚ
وَسَيَحْلِفُونَ بِٱللَّهِ لَوِ ٱسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا مَعَكُمْ
يُهْلِكُونَ أَنفُسَهُمْ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَٰذِبُونَ ﴿٤٢﴾

43. Mwenyezi Mungu amekuwia radhi (amekusamehe). Kwa nini umewapa ruhusa? (Ungengoja) mpaka wanaosema kweli wakupambanukie, na uwajue waongo.

عَفَا ٱللَّهُ عَنكَ لِمَ أَذِنتَ لَهُمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ
لَكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ وَتَعْلَمَ ٱلْكَٰذِبِينَ ﴿٤٣﴾

---

wanauzidishia mezi mingine kusudi, ili ikawie kufika.

39. Wanatahadharishwa wanaofanya woga kwenda vitani.

40. Hapa inatajwa namna alivyokuwa Mtume peke yake — yeye na Sayyidna Abubakr tu — siku walipokuwa wanakimbia Makka wanahamia Madina. Wakajificha siku tatu peke yao ndani ya pango la jabali.

Basi mwema asivunjike moyo akiwa peke yake au ana wachache, akiendelea na jitihadi yake, mwisho atashinda apatie chungu ya wafuwasi kama alivyopata Mtume.

43. Katika mwaka wa 9 wa *Al Hijra* Warumi waliokuwa wakitawala Shamu walizatiti vita kuja kumpiga Mtume. Basi Mtume akazatiti naye jeshi la kwenda kukabiliana nao. Vita vilikuwa vya khatari kubwa kabisa. Vita vya kwenda kukabiliana na Warumi ambao ndio waliokuwa wafalme wa zaidi kuliko nusu ya ulimwengu ulikuwa ukijulikana wakati huo. Hapana watu waliokuwa wakiweza kukabiliana na Warumi isipokuwa Waajemi. Hizi ndizo zilizokuwa dola kubwa kabisa za wakati huo.

Basi ikawa safari hii Mtume akabiliane nao. Masahaba wengi waliokuwa hawana Uislamu thabiti walijikurupusha kwenda katika vita hivi; bali hata baadhi ya wale wenye Uislamu thabiti, walijipurukusha nao; hata ndiyo maana wakaambiwa maneno yaliyomo katika Aya ya 38 ya Sura hii. Bali na Aya nyingi zilizofuatia hapa; zote zinasema habari ya vita hivi na yaliyotokea kwa ajili ya vita hivi.

Kama hii Aya ya 43 inavyoonyesha namna hao Waislamu walivyokuwa wanakuja kwa Mtume kutoa nyudhuru za uwongo kuomba wapewe ruhusa wasihudhurie vitani. Na Mtume alikuwa akimpa ruhusa asihudhurie kila anayemtaka ruhusa. Basi hapa Mwenyezi Mungu anamlaumu kuwa ya nini anampa ruhusa kila anayemtaka. Angempa ruhusa yule anayemwona kuwa ana udhuru wa kweli, si kila mwenye kuja kusema uwongo wake tu.

44. Hawatakuomba ruhusa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. (Hawatakutaka ruhusa) kutoipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anawajua wanaomcha.

لا يستأذنك الذين يؤمنون بالله واليوم
الآخر أن يجاهدوا بأموالهم وأنفسهم
والله عليم بالمتقين ﴿٤٤﴾

45. Wanakuomba ruhusa wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na nyoyo zao zina shaka; kwa hivyo wanasitasita kwa ajili ya shaka yao.

إنما يستأذنك الذين لا يؤمنون بالله
واليوم الآخر وارتابت قلوبهم فهم
في ريبهم يترددون ﴿٤٥﴾

46. Na kama wangalitaka kutoka (kwenda vitani) bila shaka wangaliandalia maandalio yake (Lakini hawakufanya lolote, ni alama kuwa hawakuwa na nia ya kwenda huko vitani). Mwenyezi Mungu hakupenda kutoka kwao (kwenda huko vitani). Na kwa hivyo akawazuia na ikasemwa (na Shetani). "Kaeni pamoja na wanaokaa."

ولو أرادوا الخروج لأعدوا له عدة ولكن
كره الله انبعاثهم فثبطهم وقيل اقعدوا
مع القاعدين ﴿٤٦﴾

47. Kama wangalitoka pamoja nanyi wasingalikuzidishieni ila mchafuko, na wangekwenda huku na huku baina yenu kukutakieni fitina (kukugombanisheni). Na miongoni mwenu wako wanaowasikiliza (watu wabaya hao). Na Mwenyezi Mungu anawajua madhalimu.

لو خرجوا فيكم ما زادوكم إلا خبالا
ولأوضعوا خلالكم يبغونكم الفتنة
وفيكم سماعون لهم والله عليم بالظالمين ﴿٤٧﴾

48. Tangu zamani walitaka kukutilieni chokochoko (na fitina) na wakakupindulia mambo chini juu, mpaka ikafika haki na kudhihirika amri ya Mwenyezi Mungu; juu ya kuchukia kwao.

لقد ابتغوا الفتنة من قبل وقلبوا لك
الأمور حتى جاء الحق وظهر أمر الله وهم
كارهون ﴿٤٨﴾

49. Na miongoni mwao yuko anayesema (kumwambia Mtume): "Niruhusu (nisije vitani) wala usinitumbukize katika fitina (kwa kuona wanawake wa huko nikafitinika nao)." Hakika wao wamekwishatumbukia katika fitina. Na kwa yakini Jahanamu itawazunguka makafiri (wasiwe na pa kutokea)

ومنهم من يقول ائذن لي ولا تفتني ألا في
الفتنة سقطوا وإن جهنم
لمحيطة بالكافرين ﴿٤٩﴾

50. Ukikufikia wema (wewe Mtume na Masahaba) unawachukiza; na ukikufikia msiba husema: "Tuliangalia vizuri tangu zamani mambo yetu (kwa hiyvo hatukufikwa na balaa hii)," na hugeuka wanakwenda zao nao wamefurahi.

إن تصبك حسنة تسؤهم وإن تصبك
مصيبة يقولوا قد أخذنا أمرنا من قبل و
يتولوا وهم فرحون ﴿٥٠﴾

51. Sema: "Halitatusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ni Mola wetu." Basi Waislamu nawamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

قل لن يصيبنا إلا ما كتب الله لنا هو
مولانا وعلى الله فليتوكل المؤمنون ﴿٥١﴾

---

Lakini Mwenyezi Mungu kwa kuona ule moyo wa Mtume ulivyokuwa mpole (rahimu) anamwambia kuwa amemsamehe kwa hayo aliyoyafanya.

46. Anabainisha Mwenyezi Mungu kuwa waongo hao, hawakuzukiwa na udhuru wowote, ila tangu zamani walitia nia wasije.

47. Inabainishwa kuwa ilikuwa kheri wasivyokuja kwani wangeharibu tu.

51. Mara nyingi Mwenyezi Mungu kasema haya Basi;

52. Sema: "Nyinyi hamtutazamii sisi ila (kupata) moja katika mema mawili (Ima kushinda tukapata ngawira au kuuawa tukapata Pepo). Na sisi tunakutazamieni kuwa Mwenyezi Mungu akufikishieni adhabu itokayo kwake au (inayopatikana) kwa mikono yetu. Basi ngojeni, nasi tunangoja pamoja nanyi."

قُلْ هَلْ تَرَبَّصُونَ بِنَآ إِلَّآ إِحْدَى الْحُسْنَيَيْنِ ۖ
وَنَحْنُ نَتَرَبَّصُ بِكُمْ أَن يُصِيبَكُمُ اللّٰهُ بِعَذَابٍ مِّنْ
عِندِهِۦٓ أَوْ بِأَيْدِينَا ۖ فَتَرَبَّصُوٓا إِنَّا مَعَكُم
مُّتَرَبِّصُونَ ﴿٥٢﴾

53. Sema: (kuwaambia hawa wanafiki): "Toeni (mali yenu) kwa kupenda au kwa kutopenda, hakutakubaliwa kwenu (kutoa huko). Hakika nyinyi ni watu maasi."

قُلْ أَنفِقُوا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا لَّن يُتَقَبَّلَ مِنكُمْ ۖ
إِنَّكُمْ كُنتُمْ قَوْمًا فَٰسِقِينَ ﴿٥٣﴾

54. Na haikuwazuilia ikubaliwe kwao michango yao, ila kwa sababu walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawafiki mahala pa kusali ila katika hali ya uvivu. Wala hawatoi (hivyo wanavyovitoa) ila kwa kuchukia.

وَمَا مَنَعَهُمْ أَن تُقْبَلَ مِنْهُمْ نَفَقَٰتُهُمْ إِلَّآ أَنَّهُمْ كَفَرُوا
بِاللّٰهِ وَبِرَسُولِهِۦ وَلَا يَأْتُونَ الصَّلَوٰةَ إِلَّا وَهُمْ
كُسَالَىٰ وَلَا يُنفِقُونَ إِلَّا وَهُمْ كَٰرِهُونَ ﴿٥٤﴾

55. Yasikufurahishe mali yao wala watoto wao. Anataka Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa hayo katika maisha ya dunia, na zitoke roho zao, na hali ya kuwa ni makafiri.

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَٰلُهُمْ وَلَآ أَوْلَٰدُهُمْ ۚ إِنَّمَا يُرِيدُ
اللّٰهُ لِيُعَذِّبَهُم بِهَا فِى الْحَيَوٰةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ
أَنفُسُهُمْ وَهُمْ كَٰفِرُونَ ﴿٥٥﴾

56. Na wanaapa kwa (jina) la Mwenyezi Mungu kwamba wao ni pamoja nanyi. Wala wao si pamoja nanyi. Bali wao ni watu wanaoogopa (ndio maana wanasema uwongo huku kwa Waislamu na huko kwa makafiri).

وَيَحْلِفُونَ بِاللّٰهِ إِنَّهُمْ لَمِنكُمْ وَمَا هُم مِّنكُمْ
وَلَٰكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَفْرَقُونَ ﴿٥٦﴾

57. Kama wangalipata pa kukimbilia au mapango au mahali (pengine) pa kuingia, (bila shaka) wangekimbilia mbio huko, wanakwenda shoti (kama mafarasi waliochafuka).

لَوْ يَجِدُونَ مَلْجَـًٔا أَوْ مَغَٰرَٰتٍ أَوْ مُدَّخَلًا
لَّوَلَّوْا إِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَحُونَ ﴿٥٧﴾

58. Na miongoni mwao (hao wanafiki) wako wanaokusema katika (kugawa kwako) sadaka. Wanapopewa katika hizo (Sadaka na Zaka) huridhika; na wakitopewa katika hayo wanakasirika.

وَمِنْهُم مَّن يَلْمِزُكَ فِى الصَّدَقَٰتِ فَإِنْ أُعْطُوا
مِنْهَا رَضُوا وَإِن لَّمْ يُعْطَوْا مِنْهَآ إِذَا هُمْ
يَسْخَطُونَ ﴿٥٨﴾

59. Na kama wangeyaridhia yale aliyowapa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakasema: "Anatutoshea Mwenyezi Mungu, karibuni Mwenyezi Mungu atatupa katika fadhila zake, na

وَلَوْ أَنَّهُمْ رَضُوا مَآ ءَاتَىٰهُمُ اللّٰهُ وَرَسُولُهُۥ
وَقَالُوا حَسْبُنَا اللّٰهُ سَيُؤْتِينَا اللّٰهُ مِن فَضْلِهِۦ

---

Wakikushituwa
Yupi awezaye
Wakiwa na lao

Wewe sishituke
Kupitisha lake
Mungu ana yake.

53. Hao wanafiki waliokuwa wakijikurupusha kwenda vitani walikuwa wakitoa pesa za misaada ili kujidhihirisha mbele za Waislamu kuwa wao ni Waislamu khalisi; na hali ya kuwa wao ni makafiri. Basi ndiyo

وَرَسُولُهُ إِنَّا إِلَى اللَّهِ رَاغِبُونَ ﴿٥٩﴾

Mtume wake (pia); hakika sisi tunaelekea kwa Mwenyezi Mungu." (Lau wangesema haya ingekuwa bora kwao).

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ
عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ
وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ
فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

60. Sadaka hupewa (watu hawa):— Mafakiri na Masikini na Wanaozitumikia na Wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu) na katika Kuwapa Uungwana watumwa na katika Kuwasaidia Wenye deni na katika (kutengeneza) Mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na katika (Kupewa) Wasafiri (waliohariblkiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

وَمِنْهُمُ الَّذِينَ يُؤْذُونَ النَّبِيَّ وَيَقُولُونَ
هُوَ أُذُنٌ قُلْ أُذُنُ خَيْرٍ لَكُمْ يُؤْمِنُ
بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِينَ وَرَحْمَةٌ لِلَّذِينَ
آمَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ
رَسُولَ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦١﴾

61. Na miongoni mwa (hao wanafiki) wako wanaomuudhi Mtume na kusema: "yeye ni sikio tu" (yaani anasikia maneno bila ya kuyapima. Waongo wakubwa). Sema: "Sikio la kheri kwenu": anamuamini Mwenyezi Mungu na anawasadiki wanaoamini (sio anawasadiki wao wanafiki). Na ni rehema kwa wale wanaoamini miongoni mwenu. Na wanaomuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu watakuwa na adhabu inayoumiza (kweli kweli).

يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ لِيُرْضُوكُمْ وَاللَّهُ وَرَسُولُهُ
أَحَقُّ أَنْ يُرْضُوهُ إِنْ كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾

62. Wanakuapieni Mwenyezi Mungu ili kukuridhisheni (japo wanamuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume), hali ya kuwa Mwenyezi Mungu — na Mtume wake (pia) — ana haki zaidi ya kuwa wao wamridhishe, ikiwa wao ni wanaoamini (ukweli).

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّهُ مَنْ يُحَادِدِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
فَأَنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا ذَلِكَ
الْخِزْيُ الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾

63. Je, hawajui ya kwamba anayeshindana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi yeye atapata moto wa Jahanamu kukaa humo daima? Hiyo ndiyo hizaya kubwa (udhalilifu inayowangojea).

يَحْذَرُ الْمُنَافِقُونَ أَنْ تُنَزَّلَ عَلَيْهِمْ
سُورَةٌ تُنَبِّئُهُمْ بِمَا فِي قُلُوبِهِمْ قُلِ اسْتَهْزِئُوا

64. Wanafiki wanaogopa kuteremshiwa sura itakayowatajia (unafiki wao) uliyomo katika nyoyo zao. Sema: "Fanyeni tu mzaha, hakika Mwenyezi

---

wanabainishiwa hapa hukumu ya mali yao hayo wanayoyatoa kwa njia ya propaganda tu.

54. Anayekufuru kwa ukaidi tu—si kwa ujinga — hayakubaliwi mema anayoyafanya. Nguvu za bure.

59. Kama kweli mtu Mwislamu basi aridhie yanayopitishwa na Sharia — aliyoyakadiri Mwenyezi Mungu na aliyoyapitisha Mtume.

60. Aya hii ni kuwakatisha tamaa hao wanafiki kuwa wao hawamo katika wanaostahiki Zaka. Wanaostahiki Zaka ni hawa waliotajwa hapa.

Na fakiri na masikini takriba ni sawa sawa; wote hawana hali nzuri; lakini fakiri hali yake ni mbaya zaidi kuliko hali ya masikini. Fakiri ni yule anayepata chini kuliko nusu ya mahitajio yake. Na masikini ni yule anayepata zaidi kuliko nusu ya mahitajio yake. Basi wote wanastahiki kupewa mpaka mahitajio yao.

Na fungu la tatu katika yale mafungu manane ya hao wanaostahiki Zaka ni "Wanaozitumikia." Nao ndio nani? Hawa ndio wale watu wanaopelekwa na Serikali kwenda kupeleleza mali ya matajiri na kuchukua kwao kinachostahiki wakapeleka Serikalini. Kisha wakawatafuta masikini na kujua hali zao wapewe Serikalini kiasi wanachohitajia.

Na "Wanaotiwa nguvu nyoyo zao" ni wale Waislamu wapya — ndio kwanza wanasilimu — na wana umma

Mungu atayatoa nje hayo mnayoyaogopa (yadhihiri kwa kila mtu)."

65. Na kama ukiwauliza (kwa nini wanaifanyia mzaha dini) wanasema: "Sisi tulikuwa tukizungumzazungumza na kucheza tu." Sema: "Mlikuwa mkimfanyia mzaha Mwenyezi Mungu na Aya zake na Mtume wake?"

66. Msitoe udhuru (wa uwongo); umekwisha kudhihiri ukafiri wenu (mliokuwa mkiuficha) baada ya kule kuamini kwenu (kwa uwongo). Kama tukilisamehe kundi miongoni mwenu (kwa kutubia kwake) tutaliadhibu kundi (jingine) kwa sababu ya kuasi kwake.

67. Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, wote ni hali moja; huamrisha yaliyo mabaya na huyakataza yaliyo mazuri, na kuizuilia mikono yao (hawasaidii mambo ya kheri); wamemsahau Mwenyezi Mungu (wamepuza amri Zake); na Yeye pia amewasahau (amewapuza). Hakika wanafiki ndio wavunjao amri.

68. Mwenyezi Mungu amewaahidi wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri, moto wa Jahanamu kukaa humo daima. Huo unawatosha (kuwaadhibu); na Mwenyezi Mungu amewalaani; nao wana adhabu itakayodumu

69. (Makafiri nyinyi ni) sawa na wale waliokuwa kabla yenu (tutakuangamizeni kama tulivyowaangamiza wao. Bali) wao walikuwa wana nguvu zaidi kuliko nyinyi na wana mali nyingi zaidi na watoto wengi zaidi kuliko nyinyi. Basi walistarehea sehemu yao, na nyinyi mnaistarehea sehemu yenu kama walivyostarehe kwa sehemu yao wale waliokuwa kabla yenu; na mkazama katika maovu kama walivyozama wao. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeruka tupu katika dunia na Akhera; na hao ndio waliokhasiri.

70. Je, Hazikuwajia, habari za wale waliokuwa kabla yao: watu wa Nuhu na Adi na Thamud, na watu wa Ibrahimu, na watu wa Madyan, na (watu wa) miji iliyopinduliwa chini juu? Mitume wao waliwajia kwa hoja zilizo wazi (wakakataa kuifuata. Basi Mwenyezi Mungu akawaangamiza); Na Mwenyezi Mungu hakuwa Mwenye kuwadhulumu, bali wao walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

إِنَّ اللَّهَ مُخْرِجٌ مَّا تَحْذَرُونَ ﴿٦٤﴾
وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ
وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ
كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ ﴿٦٥﴾
لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ ۚ إِن
نَّعْفُ عَن طَائِفَةٍ مِّنكُمْ نُعَذِّبْ طَائِفَةً
بِأَنَّهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿٦٦﴾
الْمُنَافِقُونَ وَالْمُنَافِقَاتُ بَعْضُهُم مِّن بَعْضٍ ۘ
يَأْمُرُونَ بِالْمُنكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ
وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ ۚ نَسُوا اللَّهَ فَنَسِيَهُمْ ۗ
إِنَّ الْمُنَافِقِينَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٦٧﴾
وَعَدَ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْكُفَّارَ
نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ هِيَ حَسْبُهُمْ ۚ
وَلَعَنَهُمُ اللَّهُ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٦٨﴾
كَالَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ كَانُوا أَشَدَّ مِنكُمْ قُوَّةً
وَأَكْثَرَ أَمْوَالًا وَأَوْلَادًا فَاسْتَمْتَعُوا بِخَلَاقِهِمْ
فَاسْتَمْتَعْتُم بِخَلَاقِكُمْ كَمَا اسْتَمْتَعَ الَّذِينَ مِن
قَبْلِكُم بِخَلَاقِهِمْ وَخُضْتُمْ كَالَّذِي خَاضُوا ۚ
أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَ
الْآخِرَةِ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٦٩﴾
أَلَمْ يَأْتِهِمْ نَبَأُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ قَوْمِ نُوحٍ
وَعَادٍ وَثَمُودَ وَقَوْمِ إِبْرَاهِيمَ وَأَصْحَابِ
مَدْيَنَ وَالْمُؤْتَفِكَاتِ ۚ أَتَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ ۖ
فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلَٰكِن كَانُوا أَنفُسَهُمْ
يَظْلِمُونَ ﴿٧٠﴾

---

nyuma yao, inatarajiwa ya kuwa akipewa huyu na kutukuzwa watasilimu hao pia.

'Na njia za Mwenyezi Mungu' ni kuzitumia fedha hizo katika kila mambo ya faida ya umma.

61. Ilivyokuwa Mtume hawadhihirishi ubaya wao — kwa akhlaki zake nzuri, walidhani kuwa hautambui ubaya wao.

71. Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake, ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na huyakataza yaliyo mabaya, na husimamisha Sala na hutoa Zaka na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَٰتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ
بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ
الْمُنكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُونَ
الزَّكَوٰةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُولَٰٓئِكَ
سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

72. Mwenyezi Mungu amewaahidi wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake (Amewaahidi) mabustani (Pepo) zipitazo mito mbele yake—kukaa humo daima—na makazi mazuri katika mabustani hayo yenye kudumu. Na radhi za Mwenyezi Mungu ndizo kubwa zaidi. Huko ndiko kufuzu (kufaulu) kukubwa.

وَعَدَ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَٰتِ جَنَّٰتٍ تَجْرِي
مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَا وَمَسَٰكِنَ
طَيِّبَةً فِي جَنَّٰتِ عَدْنٍ ۚ وَرِضْوَٰنٌ مِّنَ اللَّهِ
أَكْبَرُ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٧٢﴾

73. Ewe Nabii! Shindana na makafiri na wanafiki na uwe mgumu kwao. Na makazi yao ni Jahanamu, nayo ni marejeo mabaya.

يَٰٓأَيُّهَا النَّبِيُّ جَٰهِدِ الْكُفَّارَ وَالْمُنَٰفِقِينَ
وَاغْلُظْ عَلَيْهِمْ ۚ وَمَأْوَىٰهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ
الْمَصِيرُ ﴿٧٣﴾

74. (Wanafiki baada ya kwisha kusema maneno mabaya juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume na dini ya Uislamu). Wanaapa kwa (jina la) Mwenyezi Mungu (ya kwamba) hawakusema, na hali kuwa wamekwishasema neno la ukafiri, na wakakufuru baada ya (kudhihirisha) Uislamu wao (wa uwongo). Na wakaazimu ambayo hawakuweza kuyafikia. Na hawakuona baya (kwa kuja Uislamu) ila ya kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake amewatajirisha kwa fadhila Zake. Basi kama watatubia itakuwa kheri kwao; na kama wakikengeuka, Mwenyezi Mungu atawaadhibu kwa adhabu iumizayo katika dunia na Akhera; wala hawatakuwa na mlinzi wala wa kuwanusuru yoyote katika ardhi (wa kuwalinda na adhabu ya Mwenyezi Mungu isiwafike).

يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ مَا قَالُوا وَلَقَدْ
قَالُوا كَلِمَةَ الْكُفْرِ وَكَفَرُوا بَعْدَ إِسْلَٰمِهِمْ وَ
هَمُّوا بِمَا لَمْ يَنَالُوا ۚ وَمَا نَقَمُوٓا إِلَّآ أَنْ أَغْنَىٰهُمُ
اللَّهُ وَرَسُولُهُۥ مِن فَضْلِهِۦ ۚ فَإِن يَتُوبُوا يَكُ
خَيْرًا لَّهُمْ ۖ وَإِن يَتَوَلَّوْا يُعَذِّبْهُمُ اللَّهُ
عَذَابًا أَلِيمًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۚ وَمَا لَهُمْ
فِي الْأَرْضِ مِن وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٧٤﴾

75. Na miongoni mwao (hao wanafiki) wako waliomuahidi Mwenyezi Mungu kuwa: "Akitupa katika fadhila Zake tutatoa sadaka na tutakuwa miongoni mwa wanaotenda mema."

وَمِنْهُم مَّنْ عَٰهَدَ اللَّهَ لَئِنْ ءَاتَىٰنَا مِن
فَضْلِهِۦ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ الصَّٰلِحِينَ ﴿٧٥﴾

76. Lakini alipowapa hizo fadhila Zake, walizifanyia ubakhili na wakakengeuka, nao (mpaka hivi sasa) wanakengeuka.

فَلَمَّآ ءَاتَىٰهُم مِّن فَضْلِهِۦ بَخِلُوا بِهِۦ وَتَوَلَّوا
وَّهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾

77. Kwa hivyo Akawalipa unafiki (kuutia) nyoyoni mwao mpaka siku ya kukutana naye (Mwenyezi Mungu), kwa sababu ya kukhalifu kwao waliomuahidi Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya kusema kwao uwongo.

فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِي قُلُوبِهِمْ إِلَىٰ يَوْمِ يَلْقَوْنَهُۥ
بِمَآ أَخْلَفُوا اللَّهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿٧٧﴾

---

67. Basi wanaokwenda mwendo huu, hata wakiwa Waislamu, watakuwa wanafiki; yawathubutikie yatakayowathubutikia.

71, 72. Sifa za Waislamu wa kweli na watakayoyapata. Mpanda wema huvuna wema.

78. Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anajua siri zao na minong'ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye mambo ya ghaibu?

79. Wale wanaowabeza Waislamu wanaotoa sadaka nyingi na (wanawabeza) wale wasiopata (chakutoa) ila kitu kidogo; wakawafanyia maskhara (mzaha). Mwenyezi Mungu atawalipa mzaha (wao), nao watapata adhabu iumizayo.

80. (Ewe Mtume)! Waombee msamaha (hao wanafiki) au usiwaombee; (yote sawa sawa). Hata ukiwaombea msamaha mara sabiini, Mwenyezi Mungu hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wavunjao amri (Zake).

81. Walifurahi walioachwa nyuma (wasende vitani. Walifurahi) kwa kule kukaa kwao nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walichukia kupigana kwa mali zao na nafsi zao katika njia (Dini) ya Mwenyezi Mungu, na wakasema (kuwaambia wenzao): "Msende (vitani) katika joto hili." Sema (uwaambie): "Moto wa Jahanamu una joto zaidi. Laiti wangefahamu."

82. Basi nawacheke kidogo (hapa duniani), watalia sana (huko Akhera). Ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

83. Basi Mwenyezi Mungu akikurudisha katika taifa moja miongoni mwao—na wakakutaka idhini ya kutoka (kwenda vitani miongoni mwa vita vitakavyotokea) — sema: "Nyinyi hamtatoka abadan pamoja nami; wala hamtapigana na maadui pamoja nami. Nyinyi mlipenda kukaa (msende vitani ile) mara ya kwanza; basi kaeni (na mara hii vile vile).pamoja na watakaobakia nyuma."

84. Wala usimsalie kamwe mmoja wao yoyote yule akifa, wala usisimame kaburini kwake (kumuombea dua). Hakika hao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakafa, na hali ni wenye kuvunja amri (za Mwenyezi Mungu).

85. Wala zisikufurahishe mali zao na watoto wao. Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwa hayo katika dunia; na roho zao zitoke, na hali wao ni makafiri.

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ
وَأَنَّ اللَّهَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ ﴿٧٨﴾
الَّذِينَ يَلْمِزُونَ الْمُطَّوِّعِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ فِي
الصَّدَقَاتِ وَالَّذِينَ لَا يَجِدُونَ إِلَّا جُهْدَهُمْ
فَيَسْخَرُونَ مِنْهُمْ سَخِرَ اللَّهُ مِنْهُمْ وَلَهُمْ
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٩﴾
اسْتَغْفِرْ لَهُمْ أَوْ لَا تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ إِنْ تَسْتَغْفِرْ
لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ ذَٰلِكَ
بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاللَّهُ لَا
يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٨٠﴾

فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ بِمَقْعَدِهِمْ خِلَافَ رَسُولِ اللَّهِ
وَكَرِهُوا أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ
فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ
قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ ﴿٨١﴾
فَلْيَضْحَكُوا قَلِيلًا وَلْيَبْكُوا كَثِيرًا جَزَاءً بِمَا
كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٢﴾
فَإِنْ رَجَعَكَ اللَّهُ إِلَىٰ طَائِفَةٍ مِنْهُمْ
فَاسْتَأْذَنُوكَ لِلْخُرُوجِ فَقُلْ لَنْ
تَخْرُجُوا مَعِيَ أَبَدًا وَلَنْ تُقَاتِلُوا مَعِيَ عَدُوًّا
إِنَّكُمْ رَضِيتُمْ بِالْقُعُودِ أَوَّلَ مَرَّةٍ فَاقْعُدُوا مَعَ
الْخَالِفِينَ ﴿٨٣﴾
وَلَا تُصَلِّ عَلَىٰ أَحَدٍ مِنْهُمْ مَاتَ
أَبَدًا وَلَا تَقُمْ عَلَىٰ قَبْرِهِ إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَ
رَسُولِهِ وَمَاتُوا وَهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٨٤﴾
وَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَأَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُعَذِّ
بَهُمْ بِهَا فِي الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٨٥﴾

---

73. Kuwafanyia ukali kidogo wabaya ni vizuri; ndio kuwatengeneza, ndio kuwaonea huruma.

74. Kuonyesha ulaimu wao; wanafanyiwa mema wanalipa ubaya.

75-79. Wanatajwa baadhi ya wabaya na baadhi ya vitendo vyao.

86. Na inapoteremshwa sura (isemayo), "Muamini Mwenyezi Mungu na ipiganieni dini pamoja na Mtume Wake," wenye wasaa na uweza miongoni mwao (hao wanafiki) hukuomba ruhusa (kutokwenda huko vitani) na husema: "Tuache tuwe pamoja na watakaokaa (wasende vitani)."

وَإِذَآ أُنزِلَتْ سُورَةٌ أَنْ ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَجَاهِدُوا مَعَ
رَسُولِهِ اسْتَأْذَنَكَ أُولُوا الطَّوْلِ مِنْهُمْ وَقَالُوا
ذَرْنَا نَكُن مَّعَ الْقَاعِدِينَ ﴿٨٦﴾

87. Wameridhia kuwa pamoja na wanaobakia nyuma; na nyoyo zao zikapigwa muhuri (zikazibwa), kwa hivyo hawafahamu (la kuwafaa ..wala la kuwadhuru).

رَضُوا بِأَن يَكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطُبِعَ عَلَىٰ
قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٨٧﴾

88. Lakini Mtume na wale walioamini pamoja naye waliipigania (dini) kwa mali zao na nafsi zao; na hao ndio watakaopata kheri; na hao ndio wenye kufuzu (kufaulu).

لَٰكِنِ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ جَاهَدُوا
بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ ۚ وَأُولَٰئِكَ لَهُمُ الْخَيْرَاتُ ۖ وَ
أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٨٨﴾

89. Mwenyezi Mungu amewatengenezea mabustani yapitayo mito mbele yake, wakae humo. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ
خَالِدِينَ فِيهَا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٨٩﴾

90. Na walikuja wenye nyudhuru (za kweli) katika Mabedui (waliokuwa Waislamu) ili wapewe ruhusa. Na wakakaa (wasije kutoa udhuru wala kutaka ruhusa kwa Mtume) wale waliomwambia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (yaani wale wanafiki wanaojigamba mbele ya Mtume na Waislamu kuwa wao ni Waislamu). Basi itawapata wale waliodumu na ukafiri wao miongoni mwao adhabu iumizayo.

وَجَاءَ الْمُعَذِّرُونَ مِنَ الْأَعْرَابِ لِيُؤْذَنَ لَهُمْ
وَقَعَدَ الَّذِينَ كَذَبُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۚ
سَيُصِيبُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٩٠﴾

91. Hapana kosa (kutokwenda vitani) juu ya wale walio dhaifu (wa umbo lao), wala juu ya wagonjwa wala juu ya wale wasiopata cha kutumia (njiani wala cha kuwaachia watu wao majumbani). (Si kosa kwao) maadamu wanamfanyia nia nzuri Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hakuna njia (ya kuwalaumu) wanaofanya mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

لَّيْسَ عَلَى الضُّعَفَاءِ وَلَا عَلَى الْمَرْضَىٰ وَلَا عَلَى الَّذِينَ
لَا يَجِدُونَ مَا يُنفِقُونَ حَرَجٌ إِذَا نَصَحُوا لِلَّهِ
وَرَسُولِهِ ۚ مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِن سَبِيلٍ ۚ
وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٩١﴾

92. Wala (hapana kosa) juu ya wale waliokujia ili uwapatie cha kupanda, (wende vitani), ukasema: "Sina cha kukupandisheni juu yake;" wakarudi, na hali macho yao yanamiminika machozi kwa huzuni ya kukosa kupata masurufu hayo.

وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لَا
أَجِدُ مَا أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ تَوَلَّوا وَّأَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ
مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا أَلَّا يَجِدُوا مَا يُنفِقُونَ ﴿٩٢﴾

93. Iko njia (ya kuwalaumu) wale wanaokuomba ruhusa (wasije vitani wala hawatoi

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ

80. Jaza yao maadamu hawakutengenea.
81, 82. Baadhi ya mabaya yao na yatakayowafika.
83, 84. Yanatajwa yakufanyiwa hawa ili waogope wengine.
86, 87. Baadhi ya mabaya ya wanafiki.
88, 89. Sifa ya Mtume na Waislamu wema na jaza yao.
90. Baadhi ya mabaya waliyokuwa wakiyafanya hao wabaya na yatakayowapata.

kitu), na hali wao ni matajiri, wameridhia kuwa pamoja na wanaobakia nyuma. Na Mwenyezi Mungu amewapiga muhuri juu ya nyoyo zao; kwa hivyo hawajui (lolote wala hawabali).

وَهُمْ أَغْنِيَاءُ ۚ رَضُوا بِأَن يَكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطَبَعَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٩٣﴾

94. Watakutoleeni udhuru mtakaporudi (mkakutana nao). Sema: "Msitoe udhuru; hatutakuamininii. Mwenyezi Mungu amekwisha kutueleza khabari zenu. Na karibuni hivi Mwenyezi Mungu ataviona vitendo vyenu (tena) na Mtume Wake (pia). Kisha (mkifa) mtarudishwa kwa Mjuzi wa ya siri na ya dhahiri, naye atakuambieni (yote) yale mliyokuwa mkiyatenda."

يَعْتَذِرُونَ إِلَيْكُمْ إِذَا رَجَعْتُمْ إِلَيْهِمْ ۚ قُل لَّا تَعْتَذِرُوا لَن نُّؤْمِنَ لَكُمْ قَدْ نَبَّأَنَا اللَّهُ مِنْ أَخْبَارِكُمْ ۚ وَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَىٰ عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٤﴾

95. Watakuapieni Mwenyezi Mungu mtakaporudi kwao (mkakutana nao), ili muwasamehe (mvapuze waliyoyafanya). Basi wapuzilieni mbali. Bila shaka wao ni najisi, na makazi yao ni Jahanamu. Ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

سَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ إِذَا انقَلَبْتُمْ إِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُوا عَنْهُمْ ۖ فَأَعْرِضُوا عَنْهُمْ ۖ إِنَّهُمْ رِجْسٌ ۖ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٥﴾

96. Wanakuapieni ili muwe radhi nao. Basi mkiwa radhi nao nyinyi (ndiyo nini maadamu Mwenyezi Mungu hakuwapa radhi?), basi Mwenyezi Mungu hawi radhi na watu wavunjao amri.

يَحْلِفُونَ لَكُمْ لِتَرْضَوْا عَنْهُمْ ۖ فَإِن تَرْضَوْا عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٦﴾

97. Mabedui wamezidi sana katika ukafiri na unafiki na wameelekea zaidi wasijue mipaka ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا حُدُودَ مَا أَنزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩٧﴾

98. Na katika Mabedui hao wako wanaofikiri kuwa wanayoyatoa (katika kusaidia Uislamu) ni gharama ya bure, .na wanakungojeleeni misiba. Misiba mibaya itakuwa juu yao (itawafika wao). Na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye.

وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَن يَتَّخِذُ مَا يُنفِقُ مَغْرَمًا وَيَتَرَبَّصُ بِكُمُ الدَّوَائِرَ ۚ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٩٨﴾

---

91,92. Wanatajwa wenye kupewa udhuru.

93. Wanatajwa wenye kustahiki lawama.

94. Tumeona katika Aya ya 81 ya Sura hii kuwa vilipoandaliwa vita vya kwenda kupigana na Warumi wale waliokuwa hawana Uislamu wa kweli walijipurukusha wasende. Wakaja wengine kutoa nyudhuru za uwongo, na wengine wakangojea huko vitani.

97. Watu wakikaa katika miji wakakutana na watu hawa na watu hawa wanajua yaliyo mema na yaliyo mabaya. Wanajua haya kwa ile taathira wanayoiona kwa mambo hayo na kwa kusikia.

Lakini watu wakikaa vichungu vidogo vidogo majangwani na maporini na mashambani hawajui haya, kwa hivyo kwao ujinga unabobea na ukaidi. Ndivyo ikaambiwa hapa 'Mabedui wamezidi sana katika ukafiri na unafiki' Na tamko hilo la *'Al Aarab'* siyo kama tamko la *'Al Arab.' 'Al Arab'*.maana yake Waarabu. Na *Al Aarab* maana yake ni kila asiyekuwa mkazi wa mji, kama vile wakazi wa porini, jangwani, mashambani na kama huko; akiwa Muarabu au Muafrika au Mzungu au Mchina au wa kabila nyingine.

Basi sivyo hivyo wanavyojivurumizia tu hao wanaojidai kufasiri Qurani—na hali ya kuwa hawajui lugha ya Kiarabu — wakaona *Al Arab* na *Al Aarab* ni maana moja na maana yake ni Waarabu. Wakasema kuwa Waarabu wamezidi sana katika ukafiri na unafiki!

Haifai kabisa kwa mtu kuifasiri Qurani pasi na kujua kweli kweli. Mwenyezi Mungu atamtia adabu kubwa

99. Na katika Mabedui hao wako wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho, na wanaitakidi kuwa wanayoyatoa ndiyo (sababu za) kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu, na za (kupatia) dua za Mtume. Sikieni! Hakika hayo ni (kweli kuwa ni) mambo ya kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu atawaingiza katika rehema Yake. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

ومن الأعراب من يؤمن بالله واليوم الآخر
ويتخذ ما ينفق قربت عند الله وصلوت
الرسول ألا إنها قربة لهم سيدخلهم الله
في رحمته إن الله غفور رحيم ٩٩

100. Na wale waliotangulia wakawa wa kwanza katika (Uislamu)—Muhajiri na Ansari, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri—Mwenyezi Mungu atawapa radhi, nao wamridhie (Mwenyezi Mungu kwa hayo mazuri atakayowapa) na amewaandalia Mabustani yapitayo mito mbele yake, wakakae humo milele. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

والسبقون الأولون من المهجرين والأنصار
والذين اتبعوهم بإحسان رضي الله
عنهم ورضوا عنه وأعد لهم جنت تجري
تحتها الأنهر خلدين فيها أبدا ذلك الفوز
العظيم ١٠٠

101. Na katika Mabedui wanaokaa pembezoni mwenu katika vitongoji vya karibu yenu hapo Madina) kuna wanafiki. Na katika wenyeji wa Madina (pia kuna wengine wanafiki); wamebobea katika unafiki; (hata) huwajui (kuwa ni wanafiki). Sisi tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa katika adhabu kubwa.

وممن حولكم من الأعراب منفقون ومن أهل
المدينة مردوا على النفاق لا تعلمهم نحن
نعلمهم سنعذبهم مرتين ثم يردون إلى
عذاب عظيم ١٠١

102. Na (wako) wengine wamekiri dhambi zao (wametubia kwa Mwenyezi Mungu, wakapokelewa). Wamechanganya vitendo vizuri na vingine vibaya. Asaa Mwenyezi Mungu akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وآخرون اعترفوا بذنوبهم خلطوا عملا صلحا
وآخر سيئا عسى الله أن يتوب عليهم إن الله
غفور رحيم ١٠٢

103. Chukua sadaka katika; mali zao, uwasafishe na kwatakasa kwa ajili ya hizo (sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombee dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe); na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye.

خذ من أموالهم صدقة تطهرهم وتزكيهم بها
وصل عليهم إن صلوتك سكن لهم والله
سميع عليم ١٠٣

104. Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja Wake na kuzipokea sadaka, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukubali toba sana (na) Mwenye rehema?

ألم يعلموا أن الله هو يقبل التوبة عن عباده
ويأخذ الصدقت وأن الله هو التواب
الرحيم ١٠٤

---

kabisa ya kumuangamiza kweli kweli Akhera au pengine papa hapa duniani kwani anamsingizia Mwenyezi Mungu asiyoyasema.

100. Malipo watakayoyapata wema—waliotangulia na wa sasa na watakaokuja.

101. Kwenye wema wake mtu na wabaya wake wako, na kwenye wabaya wake na wema wake wapo pia. Kheri tupu kabisa haipatikani. Basi hata huko Madina alikopokewa Mtume namna hiyo kwa kichwa na mikono na miguu, na walikuwa wengine katika hao ni maadui zake kweli kweli, ila wanajidhihirisha tu mbele yake na mbele za watu wake kuwa wao wanamfuata Mtume na kumpenda na kupendelea ya kheri. Kumbe waongo.